AAP 51 (1997):23-54

# KIZIWI, KIPOFU NA KILEMA: UBAGUZI AU HESHIMA?

ABEL Y. MRETA, THILO C. SCHADEBERG na GERLIND SCHECKENBACH

"The deaf, the blind and the lame: discrimination or respect?" In this article we investigate what the assigment of these (and other) words to the KI-class means. We depart from the common explanation which says that the KI-class here signals contempt since it is not the typical class for human beings in Swahili. We then analyse the surprisingly large corpus of nouns referring to people in the KI-class and show how they got assigned to this class. This leads us to a more general statement about the meaning of a noun class. The final section is a case study of one particular word, *kigego,* and what it formerly stood for in Vuasu (Upare) and other societies bordering the Swahili world.

## 1. Utangulizi

Wanafunzi wa Kiswahili hushangaa wakijifunza maneno kama *kiziwi, kipofu* na *kilema.* Wakati wanapokuta maneno haya wameshajua kwamba majina yawakilishayo watu huwa katika ngeli za MU/WA au pengine hukosa kiambishi awali cha ngeli, k.m. *baba* na *askari.* Wanafikiri pia kwamba majina katika ngeli za KI/VI kwa kawaida huwakilisha vitu, yaani vitu visivyo na uhai. Kwa hiyo wanafunzi na walimu wao hujaribu kueleza maneno kama *kiziwi, kipofu* na *kilema* kama ni aina ya ubaguzi: maneno haya—inasemwa—yanataja watu hawa kama si watu bali ni kama vitu. Hivyo ndivyo alivyosema Meinhof (1906:12-13):

> Ngeli ya *iki* tangu zamani inajulikana kama ni ngeli ya 'desturi', 'matumizi' na 'chombo', k.m. *Kiswahili, kizungu, kifuniko, kidole* (kinachofikiriwa kama chombo).
>
> Kutokana na maana 'desturi, namna' kumetokea matumizi ya kiambishi hicho kwa kutaja mambo yasiyoshikika ("mambo dhahania"), k.m. *kilio, kipunguo.*
>
> Mtu anayetajwa kwa jina lenye kiambishi hicho cha kitu hudharauliwa. Kwa hiyo vilema na watu kadhalika huwa katika ngeli ya KI: *kipofu, kiziwi, kilema, kipumba.*[1]

Bila shaka walimu wenzetu wa kizungu wote wameshayasikia maoni hayo hata kama wamefundishwa Kiswahili kwa kutumia vitabu visivyotaja maelezo hayo. Unaweza kukuta

---

[1] "Die 7. Klasse *iki* ist 1. in ihrer Bedeutung als "Sitte, Gebrauch, Werkzeug" schon früh erkannt, z.B. Suaheli *ki-suaheli* ..., *kizungu* ..., *kifuniko* ..., *kidole* 'Finger' (als Werkzeug betrachtet). ...

2. Aus dem Begriff "Sitte, Art und Weise" entwickelt sich die Verwendung des Präfixes zur Bezeichnung von Abstrakten.
z.B. Suaheli *kilio* ..., *kipunguo* ...

Wird eine Person mit diesem Sachenpräfix versehen, so wird sie dadurch verächtlich behandelt. Darum gehen Krüppel u. ä. nach Kl. 7.
Suaheli *kipofu* ..., *kiziwi* ..., *kilema* ..., *kipumba* ...

Als "Schmähpräfix" nähert es sich dem Verkleinerungspräfix, mit dem es im Swahili ganz zusammengefallen ist unter Mitwirkung der Lautähnlichkeit von *ki* und *ka* s. Kl. 13."


maoni hayo kila mahali, k.m. katika sarufi ya Polomé (1967:100[2]). Baadhi ya wataalamu wa elimu ya jamii hufuata maoni ya wana-isimu na kufikiri kwamba ubaguzi wa vilema unasababishwa na lugha ya Kiswahili.

Lakini, iko njia nyingine ya kueleza kwa nini maneno hayo yamo katika ngeli ya KI. Tunajua kwamba ngeli ya KI inatumika kuunda nomino zenye maana ya 'namna', k.m. *kienyeji* kinaundwa kutoka na neno *mwenyeji* na kuwakilisha namna wenyeji wasemavyo au wavaavyo au wapikavyo au tabia yoyote yao. Hivyo, tungeweza kusema kwamba neno kama *kipofu* kinawakilisha, kimsingi, namna ya mtu fulani, hakiwakilishi utu wake kamili. Hivyo alivyofundisha hayati Sheikh Salum Kombo, mwaka wa 1964, huko katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Alivyoona yeye, kusema *kipofu* badala ya **mpofu* si dalili ya ubaguzi, bali ni njia ya kutoa heshima.

Bila shaka tunakubali kuwa maoni hayo ni mema na ya kuvutia sana. Kwa bahati mbaya, usahihi wa kisiasa, yaani *political correctness,* peke yake si hoja ya kutosha katika uchunguzi wa maana. Maelezo yote mawili tuliyoyataja yawezekana, lakini moja tu yaweza kuwa ni kweli. Lakini lipi?

## 2. Mitandao ya maana kwa ngeli ya KI


Zaidi ya karne moja sasa, wataalamu wa Kibantu na wa Kiswahili wamejaribu kueleza maana za ngeli kama ni mitandao ya maana. Kila "wavu" wa aina hii ni vijopo vya maana mbalimbali zinazozunguka maana moja ambayo iko katikati. Maana hii ya msingi kwa Kiingereza inaitwa "prototype". Pengine tunaambiwa kwamba hii maana ya msingi ni kitu kipya (taz. Givón 1986) lakini hata istilahi "prototype" ilitumiwa na Sacleux (1909:66). Mitandao mingi ya aina hii imebuniwa, na kwa kawaida hufanana sana. Tuangalie mifano mitatu tu. Tumeshauangalia mtandao wa Meinhof (1906:12–13) ambao tunafikiri ni wa kwanza kuhusu lugha za Kibantu kwa jumla pamoja na kutoa mifano ya Kiswahili.




[2] "*kipofu* 'blind', *kiziwi* 'deaf', *kilema* 'cripple', etc.—evidently with a derogatory connotation, the use of the typical prefix for things pointing to their being of no account as living beings in a definite social context."

Anavyoona Meinhof, maana ya msingi ni 'desturi/matumizi/chombo', tena anasisitiza kwamba maana hii ilikuwa imejulikana tangu zamani. Kwa Meinhof, maana za maneno hayo zilikuwa ni karibu sana; neno la Kijerumani *Gebrauch* ina maana ya 'matumizi' na vile vile siku za Meinhof lilikuwa na maana ya 'desturi'. (Linganisha na Kiingereza *use* na *use to* au *usual.*) Kutoka kwa maana hiyo ya msingi imeota maana ya pili, yaani "isiyoshikika". Tukiangalia mifano yake, afadhali angetumia "kitendo" badala ya istilahi yake "abstrakt". Tumeshasikia maelezo ya Meinhof juu ya maneno kama *kipofu,* lakini haelezi kwa nini sasa ngeli ya KI imekuwa ni "ngeli ya vitu". Labda anafikiri kuna hatua ndogo tu kutoka 'chombo' hadi 'kitu', au pengine anafikiri juu ya maneno *mtu* na *kitu* yanayotajika mno. (Dosari ya mfano huu ni kwamba maneno hayo yana uhusiano wa pekee, hakuna jozi nyingine ya maneno inayofanana na jozi hii.) Hatujui hoja zake, lakini anaeleza maana ya ubaguzi kama ni matokeo ya kuunganisha maana ya *kitu* na maana ya *mtu.* Mwishowe, Meinhof anaona uhusiano baina ya maana ya *ubaguzi* na maana ya udogo; kwa upande mwingine anaelewa kwamba matumizi ya ngeli ya KI yenye maana ya udogo ni kitu kipya katika Kiswahili na kwa hiyo hayawezi kueleza asili ya maneno kama *kilema.*

Mtandao wa kwanza kuhusu maana za ngeli hasa za lugha ya Kiswahili ulibuniwa na Sacleux (1909; ngeli za KI/VI k. 65-68).





Kufuatana na Sacleux, kiini cha ngeli KI ni 'kitu'—neno hilo yeye mwenyewe analiita "prototype"[3]. Kutokana na neno hilo anapata maana ya msingi 'namna', kwa hiyo anaiita ngeli hii "ngeli ya namna" ("genre modal"). Baadhi ya mifano yake ni *Kiswahili, kimya, kilema* na *kifunguo.* Hatua ifuatayo ni kuunga maana ya namna na maana ya udogo, na maana hii ya udogo inaingia pamoja na maana ya dharau. Anavyoeleza, majina ya watu yanaweza kuingia ngeli hii kwa sababu mbili: wengine ni udogo, wengine ni kama chombo, k.m. *kiongozi.*

Hivyo, tunapewa maelezo mawili kuhusu maneno kama *kilema* na *kiziwi.* Kwanza, Sacleux anataja *kilema* kama ni mfano wa 'namna', na baadaye anataja *kiziwi* kama ni mfano wa ubaguzi.

[3] Sacleux 1909:66: "Le mot *ki* «quelque chose, quoi», conservé dans un certain nombre de langues [...], semble avoir été le prototype du préf. *ki-*." Labda alirejea kwenye neno la kuswali **-ki,* kwa Kiswahili *-pi.*

Wataalamu wengi wengine wamependekeza mitandao ya maana za ngeli za Kibantu na za Kiswahili. Mwisho ni pendekezo la Contini-Morava (1995). Tunakariri picha ya mtandao wake wa ngeli ya KI bila ya kutafsiri Kiingereza chake.




Kuna tofauti mbalimbali baina ya mtandao huu wa Contini-Morava na ile ya Meinhof na Sacleux. Tofauti ya kwanza ni kwamba hakuna mahali maalum kwa udogo, maneno ya aina hii hayaonekani kama ni kundi moja. Tofauti nyingine ni kwamba maana ya 'kufanana' au 'namna' inapata cheo cha chini kabisa. Kufuatana na Contini-Morava, 'namna' ni sitiari inayotoka kwa 'sehemu ya dutu ("substance")' kwa njia ya "aina na wingi" ("quality and quantity"), tena 'sehemu ya dutu' ni sitiari kutoka kwa 'sehemu ya kitu'. Nilishangaa kusoma kwamba Sharifa Zawawi (1979) anatajwa kama ni mtaalamu wa kwanza aliyegundua kwamba maana ya ngeli ya KI ni 'namna'.

Kuhusu watu walemavu, Contini-Morava anaamini kwamba "maneno haya kwa kawaida ni yenye maana ya ubaguzi'[4]. Anavyoona, maneno hayo ni kundi moja tu la "vitu vinavyofupishwa ama kwa kutumiwa mno au kwa kukatwa". Tena hachori mstari baina ya kundi la walemavu na kundi la sehemu za mwili zenye ugonjwa, ijapo kuna maneno mengi yenye maana hizi mbili.

Basi, tumeona kwamba njia zaidi ya moja zimebuniwa kwa watu walemavu kuingia ngeli ya KI. Kutoka kwa *kitu* tunafika kwenye *si mtu kamili;* kutoka kwa *udogo* tunaweza kufika

[4] Contini-Morava 1995: "These latter terms generally have derogatory connotations in Swahili."

kwenye *thamani ndogo;* na kutoka kwa *namna* tunaweza kupitia *ulemavu* na kufika hadi *mlemavu.* Lakini bado hatujapata hoja ambazo zingetusaidia kuchagua baina ya maelezo hayo. Je, kila mtaalamu anaweza kuchora mtandao wake na kubuni mahusiano ya kimaana anavyopenda?

## 3. Aina za watu katika ngeli ya KI

Mpaka kufikia hapo imezungumziwa tu kuhusu walemavu kama mfano pekee wa watu wanaowakilishwa katika ngeli ya KI. Pia tumesikia kwamba uhusiano uliopo kati ya kundi hili la watu walemavu na maana ya ngeli ya KI umejitokeza katika namna na njia mbalimbali. Inafaa kutenganisha kwa upande mmoja wazo la kuwa ngeli ya KI ikiwarejea watu, ni watu wenye vilema hasa, na kwa upande mwingine, madai kuwa ngeli ya KI inayo maana yake maalumu, ikiwemo pia maana inayorejea kwa watu walemavu. Tunaona ni muhimu kila dai lizungumziwe kipekee. Ili tupate msingi katika kufikia hitimisho kwenye kazi hii inahitajika kanzi ya data ipanuliwe.[5]

Tunaanza kwa kuuliza maswali yafuatayo: Je, kuna maneno mengine yaliyopo katika ngeli ya KI yawakilishayo watu tukiacha yale yaliyotumika kuwataja watu walemavu? Kama yapo ni kiasi gani, na yana maana gani, pia yalinyambuliwa namna gani kiumbo na kimaana? Baada ya hapo tutayaangalia majina yawakilishayo watu walemavu ili kuona kama njia za kuyaunda ni tofauti na yale mengine yanayowataja watu katika ngeli ya KI. Tukifikia hapo ndipo swali la maana ya ngeli litaulizwa kwa upya.

Ukusanyaji wa maneno yaliyopo katika ngeli ya KI hasa yale yanayowarejea watu ulifanyika kwa kuzichambua kamusi mbalimbali za Kiswahili kuanzia kamusi ya zamani ya Krapf (1882) hadi kamusi za siku hizi. Kwa njia hii tumeweza kushuhudia mabadiliko ya kimatumizi ya maneno mbalimbali kwa zaidi ya miaka mia moja. Kamusi nyingine zimeonyesha mifano ya matumizi ya maneno hayo katika sentensi, lakini sehemu nyingine ilibidi mifano ya ziada iliyopatikana kutoka katika marejeo mbalimbali iongezewe. Katika makusanyo yetu ya maneno, tumepata maneno machache yanayowarejea watu ambayo yanatumiwa na wasemaji wa lugha hii na hata pia katika vyombo vya habari, lakini bado hayajaingizwa katika kamusi. Tulitazama pia maana mpya kutoka kwa yale maneno ya zamani.[6]

Kwa kanzi yetu ya msamiati tumechukua maneno yote katika ngeli ya KI yanayomrejea mtu. Katika maneno hayo hayahusiki tu yale yanayotumika moja kwa moja kumtaja mtu, k.m. *kiongozi,* bali kuna maneno yale pia yanayomrejea mtu ambayo kwa ujumla ndiyo mengi zaidi, k.m. *kichocheo* 'kitu chochote kinachotumiwa kwa kukolezea moto' (TUKI 1981), 'mtu mchochezi' (Sacleux 1939; Höftmann 1979), na siku hizi pia 'kisababishi' kutoka kwa maana ya 'catalyst' (TUKI 1996). Hapa tunajua kuwa kimsingi ngeli ya KI si ngeli inayohusika na watu, hivyo inabidi tuwe waangalifu katika kuzichambua tamathali za usemi zinazofanya neno liwakilishalo kitu kingine limrejee mtu katika ngeli hiyo.

[5] Diski ya kompyuta yenye kanzi ya data inapatikana kutoka kwa mwandishi GS, Chuo Kikuu cha Bayreuth.

[6] Hapa pia tunawashukuru Bw. Wamitila kutoka Kenya na Bw. Fauz kutoka Tanzania kama wasemaji wa lugha hii walitusaidia kutokana na ujuzi wao.

Majina yanayoonyesha hali ya udogo ni muhimu vilevile katika uchambuzi wa majina yawakilishayo watu katika ngeli ya KI. Majina yenye maana hiyo ni sehemu kubwa ya maneno yaliyomo katika ngeli ya KI, na mengineyo yanawarejea watu, k.m. *kibaba, kijibwa*. Tunaona kuwa mara kwa mara majina hayo hayaonyeshi hali ya udogo tu, bali yamefungamana pia na mabadiliko ya maana ambayo ndani yake inamrejea mtu: *kibaba* ni 'mtu asiyetekeleza wajibu wake kama baba', *kijibwa* ni 'mtu mnyonge anayetumiwa na mabeberu kwa faida yao; kibaraka' (TUKI 1981). Katika kanzi yetu ya msamiati, tumechukua maneno yale yote yanayoonyesha hali ya udogo na kuwarejea watu mradi tu yameingizwa kwenye kamusi. Na katika uchambuzi wetu tumeacha maneno yale tu yanayoonyesha majina kamili pamoja na yale machache tuliokuwa na mashaka nayo.

Kati ya maneno yanayowarejea watu, mengine yana maana zaidi ya moja, tulivyoona katika neno *kichocheo*. Mifano mingine iliyoonyesha polisemia ni kama: *kijogoo* '1. mtu shujaa; hodari. 2. mtu anayependa wanawake sana' (TUKI 1981), na *chura* 1. 'mtu anayefanya kazi ya kusafisha vyoo' (Bakhressa 1992; Baba Malaika 1994); 2. 'mtu, hasa mwanaume, mwenye tabia ya kubadilishabadilisha mazingira yake kulingana na jinsi anavyofasiliwa na mwanamke'[7]. Kila maana itokanayo na polisemia imeangaliwa kipekee.

Tumekusanya kanzi ya msamiati wa majina 247 yanayowarejea watu katika ngeli ya KI, pamoja na polisemia, tumebainisha jumla ya vitomeo 262. Kwa kweli kiwango kikubwa hivi cha makusanyo kimetushangaza kwani hatukutegemea kuwa karibu 10% ya nomino zote zinazopatikana katika ngeli ya KI zinawakilisha watu. Lakini inabidi kusema kwamba karibu 20% ya maneno yanayorejea watu katika kamusi mbalimbali hayafahamiki kwa wasemaji wa lugha hii siku hizi. Sababu zinazoweza kutolewa ni kwamba: (i) Kiasi cha maneno yamekuwa ni yale yaliyotumika zamani. (ii) Maneno mengine yanatoka katika lahaja za Kiswahili hasa zile la kaskazini.

Majina yawakilishayo watu katika ngeli ya KI sio kwamba tu yapo tele, bali maana zake pia zipo kwa wingi na haziwarejei watu walemavu tu. Idadi ya maana za majina ya watu katika ngeli ya KI zitajidhihirisha vizuri wakati hayo maneno yatakapogawanywa katika vijopo vya maana. Maneno hayo tumeyapanga kama tulivyofikiri wenyewe, pia jinsi maneno yenyewe yalivyohusiana. Vilijitokeza vijopo 15 vya maana na kifungu kidogo cha WABAKIO kwa ajili ya maneno yasiyoweza kuainishwa katika vijopo vilivyojitokeza.

**Vijopo vya maana** (vitomeo 262 = 100%):

| | | |
|---|---|---|
| TABIA | 29% | mwenye tabia: nomino hizi zinarejea hali au sifa ya mtu ambayo ndiyo picha halisi ya mtu huyo (k.m. *kichocheo*) |
| KASORO | 12% | mwenye kasoro: watu wenye vilema mbalimbali au upungufu au dosari fulani katika mwili |
| KIJUMBE | 9% | watu wanaotumiwa na watu wengine kama chombo au pia mtu anayejipendekeza kwa watu ambao anafikiri anaweza akafaidika kutoka kwao (k.m. *kibaraka*) |

[7]Linganisha wimbo wa chura ulioimbwa na kikundi cha taarab cha JKT.

| | | |
|---|---|---|
| MWENENDO | 8% | mwenye mwenendo: ni nomino zinazorejea mazoea fulani ya mtu ambayo hutajwa kuwa ndiyo ufafanuzi halisi wa mtu huyo (k.m. *kirukanjia*) |
| KIGOLI | 7% | watoto na vijana: kijopo hiki kidogo kinapakana na kijopo kingine cha maana katika ngeli ya KI ambacho kinahusisha viumbe ambavyo havijafikia hatua ya kuzaliwa (k.m. *kiini, kijusi, kilenge*) |
| KIFUNDI | 6% | cheo fulani kinachomrejea mhusika kikiwakilishwa kama kichekesho (k.m. *kibalozi*); kama ni kazi inapewa thamani ndogo na watu wengine |
| KIJIMO | 5% | watu wafupi sana (k.m. *kibirikizi*) |
| KIZAZI | 5% | mfuatano wa vizazi mbalimbali na pia mfuatano wao katika kuzaliwa (k.m. *kijukuu, kifungua mimba*) |
| KIPENZI | 5% | maneno ambayo hasa wanaume huyatumia kuwataja wanawake warembo; mara nyingi huwa ni maneno yanayotumiwa na wapenzi (k.m. *kimwana*) |
| UMBILE | 3% | mwenye umbile (k.m. *kiboko*) |
| KICHWA | 3% | watu mashuhuru na hodari katika jamii (k.m. *kinara*) |
| JAMAA | 2% | wajibu katika familia (k.m. *kibaba*) |
| KIZEE | 1% | watu wazee sana (k.m. *kikongwe*) |
| ASILI | 1% | watu ambao chanzo chao ni mahali fulani; maneno hayo hutumika pia kuonyesha hali ya udogo (k.m. *Kibanyani*) |
| KIZIMWI | 1% | watu katika hali isiyo kawaida: kijopo hiki kinapakana na kijopo kingine katika ngeli ya KI nacho ni PEPO (k.m. *kizuu*) |
| WABAKIO | 2% | *kidurenge* Jeune femme abandonnée par son mari, lequel redevient par ce fait *barobaro* «jeune homme» (Sacleux 1939)<br>*kiinimacho* a great sorcerer who professes to be able to blind the pupil of the eye, and to render himself invisible. He can carry off a man's property in his presence without his knowing it. (Krapf 1882)<br>*kijitu* dim. a little man. Also in contempt, manikin, or in disgust, e.g. *ewe kijitu kiovu!* Oh, you wicked wretch! (Johnson 1939)<br>*kilenge* 1. mjamzito mwenye mimba ya miezi minne. 2. mimba changa ya miezi minne (Bakhressa 1992)<br>*kimasikini* Dim. de *masikini,* «pauvre» (Sacleux 1939)<br>*kimondo* mtu mjinga (TUKI 1981) |

Majina yawakilishayo watu katika ngeli ya KI hayatoi maana moja pana tu, bali huonyesha pia maana na tathmini zinazotofautiana katika kijopo hicho cha maana. Kwa mfano katika upande mmoja kuna kijopo KIFUNDI ambacho kina watu ambao utendaji wao wa kazi au utimizaji wa

wajibu walizopewa unatiliwa mashaka na watu, k.m. *kiaskari, kibaharia, kibalozi, kikarani* (Sacleux 1939) na kwa upande mwingine kuna kijopo cha maana KICHWA ambacho kinahusu watu mashuhuri katika jamii, k.m. *kichwa, kigogo, kinara, kingunge*[8], *kiongozi, kitangulizi.*

Ugawanyaji wa vitomeo vya kanzi ya msamiati katika vijopo vya maana umeonyesha kwa upande mmoja kijopo kimoja kikubwa TABIA na vingine vidogo ambavyo vinahusiana sana kimaana. Vijopo vidogovidogo vya maana vimo pia ndani ya hicho kijopo kikubwa TABIA. Tunatoa mfano wa kijopo kidogo cha "wafitini" kwa kirefu na kutaja mifano mingine.

*chakubimbi* sabasi; mchongezi; mfitini. Bibi yule ch. amewafitinisha majirani wote mtaani (Bakhressa 1992)

*kichocheo* Brouillon, mtu wa kutia fitina (Sacleux 1939); streitsüchtiger Mensch (Höftmann 1979)

*kichochezi* mtu anayefanya watu wagombane

*kidomodomo* 1. mtu anayesengenya watu. 2. mfitini; fatani; sabasi (Bakhressa 1992)[9]

*kilimilimi* 1. hali ya kusikiliza maneno na kuyapeleka huko na huko; umbeya; udaku. 2. mtu anayeingiliaingilia maneno ya watu na kuyapeleka huko na huko; mbeya; mdaku. (TUKI 1981)

*kitatange* a cheat (Steere 1885); mtu anayegombanisha wengine; mchochezi: Umegeuka k. wachungia wenzio demani; Huyu ni k. atakutosa demani m.y. atakutia katika hatari kisha yeye atoke. (TUKI 1981)

*kipara-moto* Sobriquet donné à une personne acariâtre (Sacleux 1939)

*kizushi* an intruder (Krapf 1982; Steere 1870); mtu anayejiingiza katika mambo; mtu anayezua mambo; mwongo: Mwana wa mtu k. akizuka zuka naye (mt). Pia mzushi (TUKI 1981)

*kizuzi* Calomniateur: syn. de mzuzi. - R. -zua (Sacleux 1939)

TABIA: Watu wasio na msimamo mmoja thabiti: *chura, kigeugeu, kinyonga, kimbaumbau, kidhabinadhabina, kirukaruka.*

KIZAZI: Vizazi vinavyofuata baada ya wajukuu: *kijukuu, kilembwe, kilembwekeza, kinwa mtuzi* (Kiamu), *kinying'inya, kitakaa* (Kigunya), *kitukutuku* (Kiamu), *kitukuu.* Mtoto wa kwanza *(kifungua mimba)* na mtoto wa mwisho *(kitinda au kifunga mimba)*—wote huwa katika kizazi kimoja. Wale waliotofautishwa kutokana na mahali walipozaliwa *(kizalia)* na mahali walipokulia *(kikulia).*

MWENENDO: *kibiritingoma, kiberenge, kisiki, kibarabara, kirukanjia* (kama ni mwanaume: *kinukamto* au *kirukamito).*

---

[8] Jina *Kingunge Ngombale-Mwiru* ni la kiongozi mwenye madaraka katika serikali na chama tawala. Mtu huyu alikuwa maarufu sana katika enzi za utawala wa chama kimoja nchini Tanzania. Alikuwa Katibu Mwenezi wa chama tawala, yaani msemaji mkuu ambapo wakati huo chama kilishika hatamu na ilikuwa ni lazima kufuata maagizo ya chama hicho hata kama hukuwa mwanachama. Kwa hali hiyo jina hili lilisikika kila pande ya Tanzania na pengine ndio chanzo cha matumizi ya neno hilo.

[9] Tofauti: 'mtu mwenye tabia ya kusemasema maneno ya kuchonganisha au ya kuingilia kati maneno ya watu' (Kamusi 1981)

## 4. Unyambuaji wa watu katika ngeli ya KI

Mpaka hapa tumegundua vijopo vya maana ambavyo katika chambuzi za awali za kisemantiki, wataalamu mbalimbali waliunganisha kama mitandao ya maana. Hatutajaribu kubuni mahusiano ya vijopo vya maana ambavyo tumevipata na kuchora mtandao wa maana. Kuna mahusiano mbalimbali tofauti yanayowezekana baina ya vijopo hivyo. Lakini tukitaka kudhihirisha mahusiano yaliyopo siku hizi kwa wasemaji inatubidi kufanya majaribio ya isimu nafsia yaliyopangwa vizuri. Tukitaka kudhihirisha mahusiano ya vijopo vya maana yaliyokuwepo kihistoria inatubidi kuchunguza etimolojia ya maneno na jinsi yalivyobadilika kimaana. Bila kufanyika uchunguzi huo msingi wa kubuni mitandao ya maana utakosekana.

Tukiendelea uchambuzi wa kanzi yetu ya msamiati tunajiuliza: Kwa njia zipi za unyambuaji wa kiumbo na wa kimaana majina ya watu yanaingia ngeli ya KI? Hizi kategoria zilizotumika zitawezesha kuona uwiano uliopo kati ya njia za kimofolojia na za kisemantiki upande mmoja, na vijopo vya maana upande mwingine.

Tumetofautisha kategoria za unyambuaji wa kiumbo zifuatazo:

| | |
|---|---|
| – | chanzo cha unyambuaji wa nomino hii hatukijui (22%) |
| asili | nomino imenyambuliwa kutoka katika nomino nyingine katika ngeli ya KI yenye umbo lile lakini haimrejei mtu |
| nomino | nomino imenyambuliwa na nomino kutoka ngeli nyingine |
| kitenzi | nomino imenyambuliwa kutoka katika shina la kitenzi |
| kivumishi | nomino imenyambuliwa kutoka katika shina la kivumishi |

Unyambuaji huu wa kimofolojia unahusisha na mabadiliko mbalimbali ya kimaana ambayo yataonyeshwa pamoja na matokeo ya ujumla. Kama chanzo cha unyambuaji wa kiumbo hakijulikani haiwezekani pia kueleza unyambuaji wa kimaana.

Historia ya unyambuaji wa maneno inaweza kuhusisha hatua mbalimbali, k.m. kutoka kwenye shina la kitenzi tunaweza kunyambua nomino katika ngeli fulani. Kutoka katika ngeli hii nomino nyingine katika ngeli ya KI inaweza kunyambuliwa. Na mwisho nomino hii katika ngeli ya KI yaweza kupata maana mpya inayomrejea mtu. Ni kanuni ya msingi katika uchambuzi wetu kuzingatia hiyo hatua ya mwisho ya kumrejea mtu tu. Neno *kitoto* lililonyambuliwa kutoka katika neno *mtoto* (ngeli ya MU/WA) ni mfano wa kategoria "nomino", lakini neno *kijibwa* 'kibaraka' limeundwa kutoka katika neno la ngeli ya KI *kijibwa* 'mbwa mdogo', kwa hiyo ni mfano wa "asili".

Tunaonyesha kwa ujumla njia kuu za unyambuaji. Maneno mengi yanayowarejea watu katika ngeli ya KI yanaonyesha unyambuaji ulio wazi. Unyambuaji unahusisha maana tu (A) au umbo na maana (B).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| A. | sitiari | 25% | *kichocheo* [chombo] | *kichocheo* [mtu] |
| | metonimia | 18% | *kinara* [kitu/mahali] | *kinara* [mtu] |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | tashbihi | 5% | *chambo* [kitu] | *chambo* [mtu] |
| B.1 | udogo | 19% | *binti* [mtu] | *kibinti* [mtu] |
| | udogo (dharau) | 17% | *fundi* [mtu] | *kifundi* [mtu] |
| B.2 | kutoka katika shina la kitenzi: | | | |
| | mtendi | 13% | shina la kitenzi + -i | *kiongozi* |
| | | | shina la kitenzi + -a | *kikausha* *kifungua mimba* |
| | mtendwa | 2% | shina la kitenzi + -e | *kiokote* [mtu] |
| B.3 | kutoka katika shina la kivumishi: | | | |
| | | 1% | *kipevu* [namna?] | *kipevu* [mtu] |

*Yahusuyo kifungu A:* Aina ya uundaji wa maneno iliyojitokeza mara nyingi sana ni ile ihusuyo maneno katika ngeli ya KI yenyewe. Maneno hayo yanamrejea mtu kwa njia ya tamathali za usemi. Karibu nusu ya maneno yote yanayowataja watu katika ngeli hii yanaundwa namna hiyo. Kuna njia mbalimbali tofauti za kuhamisha maana. Kati ya hizo tumebainisha njia tatu: metonimia, sitiari na tashbihi.[10]

Metonimia inaonyesha mahusiano halisi na wala siyo ya kidhanifu kati ya mtu na maana mpya iliyokusudiwa. Kwa mfano: *kinara* ni 'kibanda kidogo kilichoinuka na hutumiwa kwa shughuli za kusomea maulidi au kuhutubia mikutano ya hadhara' (TUKI 1981). Kibanda hicho ambacho kimetumiwa kwa ajili ya kuhutubia, maana hiyo imehusishwa na mhubiri, na baadaye maana imepanuka zaidi na imemtaja kama 'kiongozi, mwenyekiti' (TUKI 1981) kwa ujumla. Mfano mwingine wa kihistoria ni ule wa kuzuka kwa neno *kibarua.* Steere (1870:59) alieleza chanzo cha matumizi ya neno *kibarua* kama ifuatavyo: "*Kibarua* is now used in Zanzibar to denote a person hired by the day, from the custom of giving such persons a ticket, to be delivered up when they are paid."

Sitiari inaonyesha mahusiano ya kimaana yasiyo halisi bali yanadhaniwa kuwa yanafanana kiumbo au kimatumizi na kile kinachorejewa. Mfano mmoja ni *kichocheo* ambao tayari tumeshautaja hapo nyuma. Mara nyingi sitiari katika ngeli ya KI zimetokana na majina ya wanyama, mifano michache ni kama *chura, kijogoo* na *kitatange* 'samaki mdogo mwenye tabia ya kuwasakiza wenziwe kwenye mtego [...] kisha yeye akatoka' (TUKI 1981). Hata hivyo sitiari nyingi zinatokana na vitu kama vile *kibarango* kumtaja mtu mfupi lakini mnene sana, au

10 Tumerejea kutoka Panagl (1978:454) fafanuzi za metonimia na sitiari.

neno *kimbaumbau* lenye maana ya 'mwiko wa pilau' lakini hutumika kwa kumtaja mtu mwembamba sana. Siku hizi hata majina ya watu yametumika kisitiari. Kuna majina mawili ya viongozi wa ngazi za juu, k.m. *kingunge* 'mtu mashuhuri' na *kihiyo* 'mtu aliyeghushi hati za kielimu'.

Tashbihi ("simile") ni tamathali ya usemi inayolinganisha mtu na kitu kingine. Lakini hakuna mahusiano ya karibu sana kati ya mtu na hicho kinacholinganishwa naye. Bakhressa (1992) alitoa mfano huu: "Katika sinema za ujasusi mara kwa mara wasichana warembo hutumiwa kama *chambo.*" Kwa kawaida tashbihi haibadilishi upatanisho wa kisarufi wa ngeli inayohusika, k.m. "kijana huyu anatumika kama *chambo cha* kunasia majambazi wenzake". Tofauti na hii tashbihi tulinganishe mfano wa sitiari iliyotoka gazetini *Motomoto:* "Vigogo wa CCM waficha mali zao" (Januari 5, 1996; taz. Mreta 1996).

Maneno yenye maana ya 'chombo' au 'kitendo' yaliyonyambuliwa kutoka katika kitenzi yanatumika hasa kama tashbihi zinazorejea watu katika ngeli ya KI, k.m., "mtu huyu ni *kifano / kigezo / kichekesho*"; "Mtume ni *kifungo cha dini*".

*Yahusuyo kifungu B.1:* Njia nyingine ya uundaji wa maneno yanayowataja watu ni ile ya unyambuaji wa majina ya watu kutoka katika ngeli nyingine ambayo yanaonyesha 'hali ya udogo' katika ngeli ya KI. Hayo ni kama theluthi moja ya vitomeo vyote katika kanzi yetu ya data. Dhana nzima ya hali ya kuonyesha udogo inatakiwa ifanyiwe utafiti wa kina zaidi ili kuweza kubainisha tofauti ndogondogo za kimaana zinazojitokeza. Mojawapo ya sababu kubwa za kutofautiana inatokana na neno la mwanzo ambalo maana ya udogo ilinyambuliwa. Kwa kiasi kikubwa maana hii ya mwanzo inafafanua pia matumizi yanayoonyesha dharau. Kwa mfano katika vijopo vya maana vya JAMAA na KIFUNDI vinahusisha watu wazima wenye wajibu mbalimbali katika familia na jamii kwa ujumla. Na jamii inategemea kuwa mhusika atatimiza wajibu huo. Ikitokea kwamba mhusika huyo hakuwajibika inavyopasa ("yupo lakini ipo kama hayupo"), basi, kwa kawaida familia au jamii itamrejea kwa jina la kuonyesha hali ya udogo kulingana na ule wajibu wake ambao hakuutimiza. Kwa mfano kama yeye ni baba wa familia watu wengine watamrejea kama *kibaba,* kama ni fundi ambaye hatendi kazi yake vizuri atatajwa *kifundi.*

Hali ya udogo inayoonyesha dharau inaweza pia kunyambulishwa kutoka katika maneno yanayowataja watu wenye tabia zisizokubalika. Watu hawa wakitajwa katika ngeli ya KI inakuwa afadhali kidogo kuliko wanapotajwa katika ile ngeli ya mwanzo, k.m. *kidaku hiki* ni afadhali kuliko kumtaja mtu *mdaku huyu.* Lakini katika hali ya kuonyesha udogo neno hilo linabakia kama tusi. Vile vile mtu anayetajwa kama *kikorofi* ni mtu mkorofi lakini ni afadhali zaidi kuliko yule anayetajwa kama *mkorofi.* Katika mifano hiyo hatuwezi kusema kwamba ni hali ya udogo inayoleta dharau.

Katika mifano tuliyoiona hapo juu hali ya udogo imenyambulishwa kutoka neno la msingi, lakini maana zinazotajwa katika mifano hiyo zinatofautiana. Katika mifano ya kwanza tunaona kuwa neno la msingi lilikuwa ni zuri na linakubalika, lakini neno linaloonyesha hali ya udogo halikubaliki. Tukija katika mifano ya pili tunaona kuwa neno la msingi halikubaliki na neno linaloonyesha hali ya udogo halikubaliki pia.

Kwa ujumla matumizi ya majina ya watu yanayoonyesha hali ya udogo yanategemea sana muktadha, kama vile maneno yaliyopo kwenye kijopo cha maana KIPENZI. Jambo lingine ambalo linahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi ni utofauti wa upatanisho wa kisarufi katika matumizi ya ngeli ya KI kuonyesha udogo, k.m. tunasema *kibinti changu* lakini *kijana wangu*; *kipusa changu* lakini *kimwana wangu.*

*Yahusuyo kifungu B.2 na B.3:* Nomino zilizonyambuliwa kutoka katika shina la kitenzi zina maana ya kisintaksia ya *mtendi* au ya *mtendwa.* Ni viambishi tamati hasa vinavyoleta maana hizo. Viambishi tamati *-i, -a* (kwenye vitenzi sababishi na vitenzi vya kauli ya kutendewa) na *-a* pamoja na kijalizo cha nomino vinaleta maana ya *mtendi* na kiambishi tamati *-e* kinaleta maana ya *mtendwa.* Majina yaliyonyambuliwa na vitenzi yamo katika vijopo vingi vya maana. Lakini mara kwa mara si rahisi kuamua kama jina fulani limenyambuliwa kutoka katika kitenzi moja kwa moja na kuingizwa katika ngeli ya KI au kama linapitia njia za tamathali za usemi. Zaidi ya hayo ni wazi kwamba majina mengine yaliyonyambuliwa kutoka katika kitenzi moja kwa moja yana maana za kitamathali, k.m. *kikausha* 'an unlucky ill-omened person, one who brings bad luck, who causes a person's property, &c., to wither, disappear, be destroyed' (Johnson 1939).

Tujiulize: Mbona nomino zenye maana ya *mtendi* au *mtendwa* zimo katika ngeli ya KI ingawa ngeli ya MTU/WATU ipo? Hatuna jibu kamili. Mapendekezo ya aina mbili yangeweza kutolewa: pendekezo la kwanza ni kwamba *mtendi* anaonekana kama *chombo.* Ingekuwa hivyo, basi, lazima kukubali kwamba njia hii ni ya kumwangalia mtu kama kitu ingawa hatuwezi kusema ni ubaguzi. Pendekezo la pili ni kwamba kuingia kwa maneno hayo katika ngeli ya KI kumechochewa kimaana kwa kufuata mfano wa neno maalum.

Nomino zilizonyambuliwa kutoka katika shina la kivumishi na kuwakilisha watu katika ngeli ya KI ni chache sana. Inawezekana kwamba hatua ya katikati inahitajika kama ilivyoonyeshwa katika mfano wa *kipevu* "Petit déluré, mûr avant l'âge [...] *mtoto huyu k.*" (Sacleux 1939).

Mara kwa mara inabidi kuangalia mfuatano wa hatua za unyambuaji kwa ukamilifu ili kuelewa vizuri hatua ya mwisho inayoleta jina la mtu. Katika kijopo cha TABIA tumegundua kwamba chanzo hicho cha kunyambuliwa jina la mtu mwenyewe ni hali, tabia na/au namna yake:

| | | |
|---|---|---|
| (Kiarabu >) | *kisirani* | *kisirani* |
| | [hali] | [mtu mwenye tabia...] |
| *mbele* | *kimbelembele* | *kimbelembele* |
| [mahali] | [tabia] | [mtu mwenye tabia...] |
| *ulimi* | | *kilimilimi* |
| *mdomo* | | *kidomodomo* |
| [sehemu ya mwili] | | [mtu mwenye tabia...] |
| *jogoo* | *kijogoo* | *kijogoo* |
| [mnyama] | [namna yake] | [mtu mwenye namna hii] |

Tunajua kwamba ngeli ya KI inatumika kuunda nomino zenye maana ya 'namna'. Katika mifano ya hapo juu nomino hizi zinarejea tabia ya mtu au namna yake. Kutoka katika 'tabia' tunarejea moja kwa moja kumtaja mtu kwa njia ya metonimia au ya sitiari.

Sasa tumeelewa njia moja muhimu inayoleta majina ya "watu wenye tabia fulani". Lakini bado linabaki swali moja: tukiangalia majina hayo, tunatambua kuwa mara nyingi sana yana maana ya dharau. Maana hiyo ya dharau ya jina la mtu imeletwa kwa njia ya metonimia kutoka katika tabia ambayo inasemekana kuwa huyu mtu anayo. Jina la mtu lililojitokeza kwa njia ya metonimia linategemea maana ya neno ambalo limetumika kwa kutaja tabia ya mtu huyu. Inaonekana kwamba tunapozungumzia tabia za watu wengine tunapenda sana kutaja tabia zao zisizokubalika. Tuseme hali ya kupata maneno mengi yanayorejea "tabia mbaya" inategemea mtazamo wetu kuhusu watu wengine na pia hoja zetu mbalimbali za kutafuta na kuyataja makosa yao. Mambo haya hayategemei ngeli ya KI na "maana" yake. Ngeli ya KI inatumika kuunda nomino zenye maana ya 'namna'. Kwa hiyo tunapata majina mengi katika ngeli hii yanayorejea namna au tabia za watu. Maneno yale yaliopo katika lugha zetu yanayotaja tabia mbaya, yamebuniwa na watu, na wala hayategemei mfumo wa lugha na mbinu zake. Ingefaa kuyachambua maneno yanayorejea TABIA katika ngeli ya MTU/WATU. Tunafikiri kwamba hatutapata matokeo tofauti na haya tuliyoyapata katika ngeli ya KI. Mbinu zinazotumika katika ngeli ya MU/WA ndizo tu tofauti, kwa vile watu wanaitwa moja kwa moja, na wala si kwa kupitia metonimia.

*Muhtasari:* Kanzi yetu ya msamiati imetuonyesha kuwa yamo majina mengi katika ngeli ya KI yanayowakilisha watu. Tukiangalia maana zake mbalimbali hatuwezi kusema tena kuwa kumtaja mtu kwa jina lenye kiambishi cha KI ni ubaguzi, kama tulivyoiona katika mtandao wa maana wa Carl Meinhof. Hata kama maana kimatilaba za ngeli ya KI zihusuzo hali ya kuonyesha 'udogo' na 'chombo' zitaongezwa, haitawezekana kuelezea kwa kinaganaga upana wa maana za majina tuliyoyapata: angalia k.m. katika ngeli ya KI yanapatikana maneno kama *kifundi* lakini vile vile *kingunge*, *kibaba* na *kibamba*, *kikojozi* na *kiongozi*, n.k.

Lakini kuona majina yenye maana nyingi tofauti yawakilishayo watu katika ngeli ya KI ilikuwa upande mmoja tu wa matokeo ya uchambuzi wa kanzi yetu ya msamiati, upande mwingine tumebainisha vijopo vidogo vya maana ambavyo vipo karibu sana kimaana. Inatubidi kueleza asili yake.

Kwa kufuata kanuni ya utaratibu wa kuchagua hatua ya mwisho katika mfuatano wa unyambuaji wa nomino iletayo jina la mtu mwenyewe, tumeona kuwa majina yawakilishayo watu katika ngeli ya KI yanatokana na vyanzo vitatu muhimu: (i) uundaji wa tamathali za usemi (metonimia, sitiari na tashbihi); (ii) unyambuaji wa hali ya kuonyesha udogo kutoka katika ngeli nyingine; (iii) unyambuaji kutoka katika shina la kitenzi unaoleta maana ya mtendi au mtendwa. Njia maalumu tuliyoigundua ya kuunda jina linalomrejea mtu kufuatana na 'namna' yake inaonekana katika kijopo kikubwa cha maana tulichokiita TABIA. Njia hii inatukumbusha maelezo ya Sacleux kuhusu ngeli ya KI kama "genre modal", yaani "ngeli ya namna".

Sasa tuangalie kijopo cha maana ya KASORO ambapo wamo watu walemavu. Je, ni njia zipi hasa za unyambuaji zinazohusisha majina yanayowarejea watu hao?

## 5. Walemavu katika ngeli ya KI

Tumebainisha maneno thelathini (30) yanayowataja watu katika ngeli ya KI, ambayo tumeyaingiza katika kijopo cha maana KASORO. Kijopo hicho hakina mipaka kamili, kama ilivyo pia katika vijopo vingine vya maana. Wanaohusishwa moja kwa moja na maana ya kijopo hiki ni watu wenye dosari fulani katika miili pamoja na hisi zao, k.m. *kiziwi, kipofu, kilema* na *kiwete*. Kando ya hao, kuna wale ambao sehemu tu ya miili yao ndiyo ina kasoro (k.m. *kibyongo, kiguru, kikono*), na wengine ni wale ambao baadhi ya vitu fulani mwilini vinakosekana kama nywele tu (*kipara*).

Wahusika wengine ni watoto wale ambao uotaji wa meno yao haukufuata utaratibu wa kawaida, nao walijulikana kama: *kigego, kibi, kileta* (taz. sehemu ya 7). Kwa ujumla jambo hilo siku hizi si muhimu tena kama ilivyokuwa zamani. Utaona pia kwamba maneno kama *kibi* na *kileta* yametoweka katika kamusi za siku hizi.

Wasemaji wa lugha hupendelea pia kumwingiza *kikojozi* katika kijopo hiki cha kasoro. Tena, katika Kiswahili kisemwacho huko Kenya utaona neno *kisukari* likitumika kumrejea mtu mwenye maradhi ya kisukari (Bakhressa 1992).

Imedhihirika kuwa watu wenye kasoro katika miili yao wapo katika ngeli ya KI. Hata hivyo inaonyesha tayari mwelekeo kwamba hata wale watu walio na kasoro fulani ambazo hazihusiki moja kwa moja na ulemavu, wamehusishwa na ngeli ya KI. Mara nyingine ngeli ya MU/WA imetumika sambamba na ngeli ya KI, kama Bakhressa (1992) anavyotuonyesha:

> "Ukimcheka yule *kigugumizi* wakati anaposema, atakasirika sana."
> "Yule ni *kichaa* na akipandwa na hamaki huvurumiza watu ngumi, basi tahadhari naye."
> "Yule mtu ni lazima awe ni *mkichaa* ama sivyo asingekuwa anatembea uchi."

Tuangalie sasa maneno yanayowataja walemavu katika ngeli ya KI yanaundwa kwa njia gani.

(i) Matokeo ya kwanza ni kwamba hakuna unyambuaji wa hali ya kuonyesha udogo kutoka katika ngeli nyingine.[11] Tunafikiri kuwa katika neno *kikojozi* ngeli ya KI hapo haionyeshi hali ya udogo, na ndivyo inavyoeleweka siku hizi. Tukiangalia upatanisho wa kisarufi tutaona pia kuwa neno hili halifuati matumizi ya ngeli ya KI kuonyesha hali ya udogo, kama mfano ufuatao kutoka Bakhressa unavyoonyesha: "Kikojozi alizungushwa mtaa mzima huku watoto wakimzoma."[12]

(ii) Tunachukulia kuwa neno *kikojozi* limenyambuliwa kutoka kitenzi na linabeba maana ya 'mtu wa aina / namna fulani'. Kando na neno hilo, tunaona pia unyambuaji wa neno *kileta (meno)* umetokea katika kitenzi. Hiyo ni mifano miwili pekee katika kijopo hiki inayomrejea mtu bila hatua ya katikati. Maana za maneno hayo hazirejei kwa chombo au kifaa, bali zinarejea moja kwa moja kwa mtendi wa aina / namna fulani ya kipekee.

---

[11] Matokeo hayo yanapinga maoni ya Contini-Morava 1995 anayeunganisha watu walemavu na "shortened things" na "immature beings".

[12] *Kikojozi*: Katika kamusi za kisasa hakuna nomino ionyeshayo ngeli ya MU tena, bali ni ngeli ya KI tu. Ngeli ya MU/WA inaonekana katika kamusi za Sacleux na Johnson ambazo tunasoma: *mkojozi, wa:* 1.

(iii) Maneno mengi yanayowataja walemavu katika ngeli ya KI hayafuati njia ya unyambuaji wa kimofolojia, bali kimsingi hufuata utaratibu wa kisemantiki.

Lakini njia ya kuunda sitiari zinazowarejea walemavu haina mifano mingi. Tuliweza kupata mifano miwili au mtiatu tu. Mifano ya sitiari ambayo tumeiona kwenye kamusi ni:

*kingune*—ni neno linalotaja miti iliyodumaa; zamani neno hili lilitumika kuwarejea watu wadogo kiumbo na waliodumaa "muashi Hamis *kingune*" (Krapf 1882). Neno hilo halifahamiki kwa wasemaji wa lugha hii siku hizi.

*kinyago*—neno hili linataja umbo fulani linaloogopesha ambalo zamani lilivaliwa kwenye sherehe za unyago. Neno hilo lilitumiwa kuwarejea watoto wachanga waliozaliwa na kasoro fulani kwenye maumbile yao.[13]

*kifefe*—neno hili ni mfano wa sitiari kama hatutaliona kama hali bali kama sehemu ya mmea: "1. uchane wa ubua. 2. mtu aliyekonda sana; mtu dhaifu sana" (TUKI 1981).

Sitiari zitokanazo na majina ya wanyama hazitumiwi kuwarejea walemavu au tuseme: hazikuonyeshwa kwenye kamusi tulizozirejea. Sitiari hizo mara nyingi zinaonyesha hali ya kutukana tulivyoona kwenye kijopo cha maana cha TABIA. Labda ndiyo sababu iliyofanya sitiari hizi zisitumike kuwarejea watu wenye vilema katika lugha ya Kiswahili.

Njia kuu ya kuunda majina yawakilishayo walemavu katika Kiswahili ni metonimia. Hapo tunaona kwamba njia hii inatudokeza kijopo cha TABIA kwa kutaja hali. Kutokana na hali fulani ya mwili tunamtaja mtu. Njia hii ya kimetonimia hujidhihirisha kuanzia hatua ya mwanzo wa neno hadi kufikia matumizi ya neno *mwenye*. Kwa mfano, *kikono* 'mkono uliolemaa' > 'mtu mwenye mkono wa aina hiyo', zamani alitajwa kama *mwenye kikono*, au ingesemekana hivi *ana kikono* (Sacleux 1939; Johnson 1939). Wakati neno *mwenye* lilipoacha kutumiwa, neno *kikono* lilitumika moja kwa moja kumtaja mtu aliyelemaa mkono.

Chimbuko la njia hii ya kuwataja watu kama ilivyoonyeshwa, tunaweza kulifuatilia zaidi. Tunaona *kikono* limenyambuliwa kutoka neno *mkono*:

| | | | |
|---|---|---|---|
| sehemu ya mwili | sehemu ya mwili yenye kasoro | mtu mwenye kasoro hii | mtu mwenye kasoro hii |
| *mkono* | *kikono* | *mwenye/ana kikono* | *kikono* |

Kwa kufuata hatua hizo hizo majina ya watu walemavu yafuatayo yameundwa: *mgongo > kigongo / kibyongo / kijongo; mguu > kigu(r)u; tumbo > kitumbo.*

Mfano wa *kitumbo* unaonyesha wazi kuwa neno hilo halirejei hali ya udogo. *Kitumbo* haina maana ya 'tumbo dogo', bali ni tumbo lililotuna kwa mbele: 'mtu mwenye tumbo la aina hiyo', 'mwenye tumbo nene' (Sacleux 1939; Johnson 1939). Hivyo ndivyo hata katika mifano mingine inafafanuliwa kuonyesha hali maalumu au ya kipekee.[14]

---

13 *Azaaye kinyago akinyonyesha.* She who gives birth to a deformed child will breastfeed it. (Scheven 1981:380)

14 Khamis (1984:17) alirejea maana hii kama "excessive, augmentative, excelling".

Lakini hatuwezi kusema kwamba ngeli yenyewe ndiyo yenye maana ya dharau. Tunajua kuwa kazi mojawapo ya ngeli ya KI ni kuunda maneno yenye maana ya 'namna' au 'hali ya kipekee'. Mara nyingi sehemu za mwili zinazotajwa kutokana na hali yake ya upekee zinakuwa ni zile zenye ulemavu fulani. Maana hii isiyopendeka inahusika na yaliyomo katika maneno yaliyotajwa, na wala sio, kule kuwemo kwa maneno hayo katika ngeli ya KI. Hoja hii tumeshatoa wakati tulipoeleza uchambuzi wa kijopo cha maana TABIA kuwa: Sisi wanadamu - tunapendelea kuzungumzia kasoro mbalimbali za watu wengine. Kasoro hizo zinahusu miili ya watu. Lakini wakati mwingine tunazungumzia pia uzuri wao wa maumbo yao, k.m. *kisura.* Tunaweza kusisitiza uzuri wa mwili na kasoro zake kwa njia hiyo hiyo ya lugha inayoleta "hali ya kipekee".

Tukirudi nyuma kuangalia vilema vya mwili tunaona kuwa, kutaja dosari fulani ya mwili inawezekana pia kwa kurejea kutoka kitu fulani: *gutu* > *kigutu* 'kipande cha kitu'; kile kilichobakia kutoka kwenye kitu kizima, k.m. kipande cha mti, tunda au pia mkono au mguu. *Vigutu* lilikuwa jina lililotumika kuwataja wale waliokatwa miguu katika zoezi la kuhesabu walemavu nchini Tanzania mwaka 1981. Maneno mengine yanayoonyesha hali ya kipekee ya mtu *(kibwiko)* au hali ya kiakili *(kichaa)* au namna na jinsi ya kuzungumza *(kigugumizi)* yamenyambulishwa kutoka kwenye kitenzi.

Tumeona kuwa mengi katika majina yawakilishayo watu katika ngeli ya KI yanapitia njia ya metonimia. Sasa ni njia zipi yanapitia majina ya watu hao ambao tunawalenga kuwa ndio kiini cha kijopo hiki cha maana: *kiziwi, kipofu, kilema, kiwete?*

Neno la *kilema* linatumiwa kutaja kasoro, aliyo nayo mtu, na pia mtu mwenyewe. Maneno *kiziwi, kipofu* na *kiwete* hayafuati njia hiyo. Siku hizi huwezi kusema: *"mtu huyu ana kiziwi / kipofu / kiwete".* Tunaweza tu kutumia neno hilo kwa mtu mwenyewe mhusika: *"kiziwi / kipofu / kiwete huyu"; "mtu huyu ni kiziwi / kipofu / kiwete".* Miaka mia moja iliyopita mambo yalikuwa tofauti. Katika kamusi na matini ya zamani tumeona, mbali na kuwataja watu, maneno hayo yalitumika pia kama ifuatavyo:

*kipofu:* *yuna kipofu cha mato* (Krapf 1882); *ana kipofu* (Velten 1910); *ana kipofu cha macho* (Sacleux 1939). Pia neno *upofu* lilikuwepo.

*kiziwi:* *asili ya kiziwi* (Ursprung der) Taubheit (Velten 1903:209); *kuwa na kiziwi* être sourd; *ukiziwi* surdité. Syn. *kiziwi* (Sacleux 1939).

*kiwete:* loss of the use of the legs (Krapf 1882, Steere 1870); *ana kiwete; kwenda kiwete* (Velten 1910), *ana kiwete, -a kiwete* (Johnson 1939)

Kwa hiyo maneno kama *kiziwi, kipofu* na *kiwete* ambayo siku hizi yanawarejea watu tu, tumeona kuwa hapo zamani yalirejea pia hali aliyokuwa nayo mhusika. Tunaona kuwa matumizi yanayofanyika siku hizi katika lugha hii ni matokeo ya uhamisho wa kimetonimia uliofanyika zamani. Asili yake imepotea.

Lakini bado tunaona matatizo. Tunacho kielelezo kimoja, ambacho kinafafanua jinsi maneno yanayowarejea walemavu yanavyotumiwa katika Kiswahili cha siku hizi. Hata hivyo hakuna tu hiyo njia moja. *Kiziwi,* kwa mfano, kama neno la kumtaja mtu mwenye matatizo ya kusikia au bubu lilishatajwa toka enzi ya kina Krapf na Steere. Lakini katika lahaja za kaskazini

lilikuwa halitumiwi. Huko walitumia *duko, maduko* (Sacleux 1939). Baadaye neno *kiduko* lilizoeleka. Tunapata mfano kutoka kwa Bakhressa (1992): "Ukisema naye huyo kiduko usipige makelele: sema kawaida naye ataelewa unasema nini." Tunadhani kuwa, neno *kiduko* limefuata mfano wa *kiziwi*, ambalo limeshaundwa na ngeli ya KI. Kama ilivyo neno *duko* na *kiziwi*, hili neno jipya *kiduko* linarejea kwa mtù tu.

Inawezekana pia kuwa kuundwa kwa neno *kipofu* kumepitia njia hiyo ya metonimia kwa kufuata mfano wa *kilema*. Kwa sababu inaonekana kuwa kabla ya kuingizwa katika ngeli ya KI, neno hilo lilikuwa katika ngeli nyingine. Lahaja ya Kimvita ilitumia, mbali ya neno *kipofu*, neno *phofu* (ngeli ya 9; Slavíková na Bryan 1973:73). Umbo hilo tunalipata pia katika hadithi aliyohariri Velten (1898:96): "...mke wangu, nimeumia macho yangu, labda ntakuwa *pofu.*" Zamani neno hilo lilitumika katika ngeli ya MU/WA pia: wakati wa Krapf watu walisema "mpofu wa mato" (angalia pia Sacleux 1939 na Johnson 1939).

Tunaelekea wapi sasa? Inabidi tuelewe kuwa hatufiki mbali kama tutakuwa tunatafuta chanzo cha maneno fulani katika Kiswahili tu. Tunachotakiwa kufanya ni kupanua upeo wetu mbali zaidi kwa kuchunguza eneo la lugha za Kibantu kuona ni maneno yapi yameenea na kutumika katika lugha nyingine na katika ngeli zipi. Tutarudia swali hilo baadaye.

Je, kutokana na uchambuzi wetu mpaka hapo tunaweza kusema nini kuhusu swali letu la kwanza: ni ubaguzi kuwataja au kuwarejea watu walemavu katika ngeli ya KI? Njia kuu ya kuunda maneno hayo siku hizi ni uhamishaji wa kimetonimia wa ulemavu na kuupeleka moja kwa moja kumtaja mtu anayehusika. Lakini njia hiyo haikufungamana tu na ngeli ya KI, kama mifano ifuatayo inavyoonyesha (Bakhressa 1992):

"*Chongo* kwa kuwa ana jicho moja anaweza kuona."
"*Matege* amekuwa katika hali hiyo tangu azaliwe."

Njia ya metonimia imedhihirisha wazi kuwa haijiambatanishi tu na uundaji wa majina ya walemavu. Hali hii inaonekana kwenye majina ya watu wengi katika ngeli ya KI. Kwa hivyo inakuwa hakuna maana kudai kwa vile istilahi za walemavu zinaundwa kwa njia ya metonimia, basi zinaonyesha tabia ya ubaguzi kwa kupitia ngeli inayohusika. Pia hali ya kwamba ngeli ya KI ni ngeli ya vitu na hali ya udogo haina uhusiano na uundaji wa maneno hayo.

Jambo la msingi kutokana na swali letu "ubaguzi au siyo?" halihusu ngeli. Maneno hayo yaliyoundwa kimetonomia yanabeba maana inayorejea kwenye kasoro ya mtu. Kutoka kwenye kasoro yenyewe tunamtaja mtu. Sisi hàtumfahamu mtu yeyote anayependa kasoro aliyonayo. Mtu huyo anaweza tu kukubaliana na hali yake, yaani hana la kufanya. Lakini hatuwezi kudhani kuwa mtu huyo anafurahi kama mtu mwingine atamtaja kwa kasoro aliyonayo.

Maoni yetu kutokana na ile tabia ya kipekee ya kuwataja watu katika ngeli ya KI katika Kiswahili kama ilivyofafanuliwa, tunaona ni ile hali ya UPEKEE na NAMNA ya mhusika. Ni hali ya kutoka katika utaratibu na kurejea kwenye hali ya upekee fulani. Wakati mwingine kunatokea hisia zinazokubalika lakini mara nyingi hisia zilizojitokeza sana hazikubaliki. Kwa ujumla: hali hiyo haihusiani na unyambuaji wa ndani kwa ndani wa lugha, bali unahusiana moja kwa moja na matakwa ya wasemaji wa lugha.

## 6. Maana ya ngeli

Tunapendekeza kwamba ungeli peke yake si lazima uwe na maana, bali kuchagua ngeli wakati wa kuunda nomino maalumu ndiko kuna maana. Kupendekeza kitu kingine zaidi ya hiki ni kutotambua namna maneno yanavyobadilika kimaana.

Tunajua kwamba neno fulani linaweza kuibua maana mbalimbali. Kwa mfano, neno la Kijerumani *Strom* kwanza lina maana ya 'mto' na kisha linaibua maana ya 'umeme'; wakati katika Kiswahili neno *umeme* kwanza lina maana ya 'miali ya moto inayoonekana kabla ya radi' na kisha linaibua maana ya 'nguvu zinazotoa cheche' (TUKI 1981). Maana za neno moja zinaweza kuachana sana hadi kuwafanya wasemaji washindwe kuona uhusiano wowote baina yake. Kwa mfano, neno *kufua* lina maana ya 'kutengeneza kitu kutokana na madini', tena lina maana ya 'kusafisha nguo kwa maji na sabuni' (TUKI 1981). Lakini wasemaji wengi hawajui neno hilo limepata maana hizi mbili namna gani. Vile vile, neno *kichwa* limepoteza uhusiano wowote na asili yake, yaani kile kichuguu kijengwacho na mchwa.

Basi, mabadiliko yayo hayo hutokea pia kwa maneno ambatani na yale yenye mofimu za unyambuaji. Kila neno lina historia yake, watu wanaweza kulipa maana mpya, yaani kuhamisha maana yake hasa kwa njia za sitiari na za metonimia. Hatimaye, sehemu za neno hilo, yaani mofimu zake, zinaweza zikapoteza maana zake za asili. Kwa mfano, neno la Kijerumani *Unterricht* lina maana 'mafunzo', lakini maana za sehemu *unter* 'chini (ya)' na *richt-* '-nyosha' zimepotea, au pengine tuseme haziko kila moja peke yake katika maana 'mafunzo'.[15] Vile vile, maana ya neno la Kiswahili *-nunua* haigawiki sehemu mbili. Hivi leo maana ya shina *-nuna* na maana ya mnyambuliko *-u-* si sehemu za maana 'kununua'.

Maneno *kiboko* na *kifaru* ni mifano mingine inayotufundisha namna sehemu za maana zinavyoweza kupotea. Contini-Morava (1995) anadokeza kwamba majina ya wanyama hawa wakubwa mno hayatarajiwi kuwa nomino za ngeli ya KI. Anaeleza kwamba "kuweka majina ya wanyama wakubwa na wenye hatari katika ngeli ya vitu vidogo vinavyoshikika labda, kitamathali, ni njia ya kufuta au kupunguza nguvu zao"[16]. Basi, japokuwa hatuna hakika lakini tungeweza kulikubali pendekezo hilo kwa sababu kuna mifano mingi mingine ya matumizi haya ya mwiko. Mfano mmojawapo ni wa neno *simba* ambalo hapo awali lilikuwa ni jina la paka mdogo wa mwituni. Sacleux (1939) anasema kwamba *kifaru* ni umbo la neno katika lahaja za kaskazini, yaani ni umbo la udogo kutoka kwa neno *faru* linalotumika katika lahaja za kusini. Kuhusu neno *kiboko* anafikiri kuwa asili yake ni neno la Kibantu **ku-boko* 'mkono', yaani maana 'kiboko' ni ya kimetonimia: "aliye na miguu minene". Sacleux haelezi kwa nini neno hilo limeingizwa katika ngeli ya KI—tuseme ni mbinu ya kusingizia kuwa ni mnyama mdogo.

---

15 Wierzbicka, baada ya kuandika juu ya maana ya "cups and mugs" kwa kirefu, anajadili nomino ambatani *paper cup* na kusema (1985:58): "The meaning of the expression *paper cup* cannot be deduced from the meanings of the words *paper* and *cup* and from the universal rule of meaning transfer based on similarity... *Paper cup* is a new lexical item, semantically related to both *paper* and *cup* but having a meaning which has to be described separately. ... Needless to say, the *wine cup* and the *communion cup,* mentioned in Webster's definition, are not cups in the sense defined here. And neither are egg cups, buttercups, brassiere cups, or hiccups."

16 "... putting names of large and dangerous animals in the class of small, manipulable things could be a way of figuratively neutralizing or diminishing their power".

Lakini dawa ya udogo hufifia upesi. Ninayataja maneno haya kwa sababu yote mawili yamezalisha maana mpya: neno *kiboko* linaweza kutumika kumrejelea mtu mnene mno, tena mkali, na neno *kifaru* hurejelea 'gari la chuma la kivita lenye mzinga' (TUKI 1981). Ni dhahiri kwamba watu walipobuni sitiari hizi waliangalia ukubwa na nguvu za wanyama hao, walilinganisha kipusa cha kifaru na mzinga, na labda walifikiri juu ya ukali wa mjeledi wa kuchapia, lakini hawakutambua maana ya udogo—sehemu hii ya maana ilikuwa imekwisha potea kabisa.

Mambo hayo yote yamejulikana kwa muda mrefu na kutumika katika uchambuzi wa kisemantiki na wa msamiati. Pendekezo letu ni hili tu: yafaa tutambue kwamba yanahusisha maana za ngeli vile vile.

Kwa upande mwingine, wakati nomino inapoundwa kutokana na kitenzi au kutokana na nomino katika ngeli nyingine, basi hakuna budi kuliweka neno hilo jipya katika ngeli fulani. Kuna aina za unyambuaji zinazotumiwa sana, na hivyo uchaguzi wa ngeli hufuata kanuni za kawaida. Bila shaka mifano bora ya kuchagua ngeli kwa uundaji wa nomino ni nomino-kitenzi, k.m. *kulea, kucheza,* na pia ngeli za mahali: *nyumbani hapa/huku/humu.* Tunaweza kusema kuwa ngeli hizo zina maana.

Kuna mbinu mbili za kawaida za kuunda nomino katika ngeli ya KI. Aina ya kwanza ni nomino za kuonyesha hali ya udogo; k.m. *kisanduku, kitoto.* (Kinyume chake, yaani hali ya ukubwa, hutumia ngeli za JI/MA, k.m. *jumba* kutoka kwa *nyumba,* na *toto* kutoka kwa *mtoto.)* Aina ya pili ni uundaji wa nomino za kuonyesha namna. Nomino hizo vile vile huingizwa katika ngeli ya KI, k.m. *kifalme, kivita, Kimvita, kisasa, kimsingi.* (Ninayachukulia maneno hayo kama ni nomino na siyo vielezi ingawa kazi yake ya kisintaksia mara nyingi ni kazi ya chagizo.)

Njia nyingine za kunyambua hazifuati kanuni za kawaida zinazotumika mara nyingi. Msemaji anayeunda nomino mpya kwa namna hii hategemei maana ya ngeli nzima—ambayo si dhahiri hata kama ni mtandao wa maana mbalimbali. Inaonekana kuwa anayebuni neno jipya hufuata mfano wa neno maalum (au pengine kijopo cha maneno machache) lenye maana ambayo inafanana sana na maana mpya anayotaka kuiwasilisha. Hii ndiyo sababu kila ngeli ina vijopo vidogo vya maneno yenye maana zilizo karibu sana. Hebu tueleze mbinu hii kwa mifano kutoka lugha nyingine.

Katika Mame-Bantu, kulikuwa na jozi ya ngeli KU/MA yenye nomino chache sana, miongoni mwake yakiwemo maneno **ku-boko,* yaani 'mkono', na **ku-gulu,* yaani 'mguu'. Kulikuwa na sababu mbalimbali za kuondolewa kwa jozi hii ya ngeli, na hasa kubadilisha ngeli yake ya umoja KU. Basi, katika lugha ya Kikinga, wasemaji walibadili neno **kuboko* likawa *ikivoko/amavoko,* tena walibuni neno jipya lenye maana 'mguu', *ikilunde/amalunde.* Cha kujiuliza ni je, kwa nini neno hilo limo katika jozi ya ngeli ya KI/MA ambayo ina nomino nne au tano tu katika lugha nzima? Sababu yake ni hii: neno la zamani **ku-gulu/ma-gulu* limegeuka kwa utaratibu ule ule wa neno la **ku-boko,* yaani likawa **ki-gulu;* baadaye shina jipya *-lunde* likabuniwa na kuingizwa katika jozi ya ngeli ya neno lililotangulia, yaani KI/MA. Kutokana na hali hiyo hatuna sababu ya kubuni maana maalumu kwa ajili ya ngeli KI/MA—kama 'mkono na mguu'.

Hapana shaka, wakati wa kuunda neno jipya, mara nyingi neno hilo hupata vigezo vya kisarufi vya neno linalobadilishwa. Mambo yayo hayo hutokea katika lugha zinazoainisha majina kwa msingi wa kijinsia, kama Kijerumani na Kifaransa. Mjerumani akisema *"eine Safari"*, neno mkopo *Safari* limerithi jinsia ya kike kutoka kwa neno la kienyeji *die Reise*, wakati katika Kifaransa, neno mkopo *le safari* limerithi jinsia ya kiume kutoka kwa neno la kienyeji *le voyage*.

Jambo lilo hilo linaonekana katika lugha ya Kiluo ambayo ni lugha ya Kiniloti inayopakana na lugha za Kibantu. Kiluo kina kiambishi awali *ra-* inayotangulia baadhi ya nomino zinazorejelea vyombo—au watu walemavu.[17] Mifano ni *radin* 'kizibo' kutoka kwa kitenzi *dino* 'kuziba', *raum* 'kifuniko' kutoka kwa *umo* 'kufunika', tena *rang'ol* 'kilema (mtu)' kutoka kwa jina *ng'ol* 'kilema (cha mwili)' na *rakuom* 'kigongo (mtu)' kutoka kwa *kuom* 'kigongo (cha mwili)'.

Lugha za Kichadi na lugha za Kiafroasia kwa jumla zinafuata mbinu iyo hiyo. Paul Newman (1980:19) alitambua kwamba "jinsi ya neno hudumu ingawa shina la neno, yaani umbo linalowakilisha maana hiyo, linabadilishwa kuwa shina jingine."[18]

Sasa tujiulize: wataalamu wanapobuni mitandao ya maana za ngeli, kwa nini wanafaulu vizuri kiasi hicho? Tulipolinganisha mitandao yao tumeona kwamba hukubaliana hasa kuhusu vile vijopo vidogo vya maana. Lakini tumeona vile vile kwamba kuna njia zaidi ya moja ya kuunganisha vile vijopo. Tena tulishindwa kuona hoja zenye nguvu kuhusu kwa nini mtandao mmoja uwe bora kuliko mwingine. Kwa kweli, kubuni mitandao hiyo ni utafiti wa kihistoria. Pengine hatua za utungaji wa maneno bado zinaonekana wazi, lakini pengine zimefichika katika kitambo cha wakati. Tukumbuke kwamba mfumo wa ngeli ni mfumo wa zama za zama, na baadhi ya maneno yamepewa ngeli zake tangu kale.

Contini-Morava (1995)[19] anawafuata wataalamu wengi wengine waliotangulia na kusema kwamba uchambuzi wa aina hii, yaani kubuni mitandao ya maana, unaonyesha kwamba makundi ya maneno yaliyomo katika ngeli fulani yamechochewa kimaana wala si kwa nasibu. Mpaka hapo tungeweza kukubali, ila tunafikiri uhusiano huu ni wa kihistoria, ambao umepotea kwa baadhi ya maneno katika lugha inavyotumiwa leo. Contini-Morava anaendelea kusema kwamba uchambuzi wa aina hii unashinda uchambuzi wa kimapokeo ambao unazingatia kwamba alama zote za kiisimu zina maana kamili. Maneno yenyewe hatuyapingi, lakini hatuwezi kumfuata mwandishi huyu kuhusu namna anavyoyatumia. Ni kweli kusema kila maana ina viwakilishi bora na viwakilishi vya wasiwasi. Kwa mfano, tuchukue maana 'nguo': kanga na kanzu ni viwakilishi bora, kofia na tai ni viwakilishi vya kando au vya mashaka. Lakini kuonyesha kwamba maana mbili zinahusiana hakulingani na kusema maana ni moja.

---

[17] Tunamshukuru Dkt. Gerrit Dimmendaal kwa kutufundisha jambo hilo. Mifano yenyewe inatoka Stafford 1967:43: "The prefix *ra-* is used before certain words to denote instruments, or persons with some peculiarity."

[18] "... the gender of a word has a tendency to remain stable even though the stem, i.e. the phonological representation of that "sememe", might be replaced by another stem."

[19] "What this type of analysis does show is that the groupings that are found are semantically motivated rather than arbitrary. In this respect it is an advance over the point of view that linguistic categories must either be definable in terms of Aristotle's necessary and sufficient conditions for membership, or dismissed as incoherent."

Kwa mfano, neno *kitoto* lina maana mbili (au zaidi?), maana moja ni 'mtoto mdogo' na maana nyingine ni 'namna ya mtoto'. Maana hizi mbili zimejibainisha, hata kama zilihusiana kihistoria.


Tunapendekeza tuendelee kutofautisha "uhusiano wa kimaana" au "motisha ya kimaana" kwa upande mmoja na "maana" yenyewe kwa upande mwingine. "Maana" ni istilahi ya kiisimu: mifumo ya kisintaksia ina maana, mofimu za uambishaji zina maana, na maneno halisi nayo yana maana. Kwa hiyo, kwa sababu kila neno lina maana yake ambayo inaweza kubadilika, sehemu za neno zilizowekwa pamoja wakati wa kuliunda neno hilo, nazo zinaweza kupoteza maana zake za asili. Hivyo huweza kutokea ngeli zisizo na maana.

Turudi kwenye swali letu la mwanzo kwamba matumizi haya ni "ubaguzi au heshima". Hivi sasa tumekwisha elewa asili ya vijopo vidogo vya maana. Katika lugha ya Kiswahili, mifano bora ya vijopo vidogo katika ngeli ya KI ni "vizazi"—na walemavu. Tumeona tena kwamba majina ya walemavu yameingia ngeli ya KI hasa kwa njia mbili: njia ya kwanza ni njia ya metonimia, yaani jina la kasoro fulani likatumika kama ni mwenye kasoro hii; njia ya pili ni njia ya "kufuata mfano". Majina ya walemavu yaliyotungwa kwa njia ya metonimia, inaonekana kwamba mengi si ya zamani sana. Kwa hiyo tutafute kiini cha kijopo chetu cha walemavu miongoni mwa maneno yaliyorithiwa kutoka lugha ya Mame-Bantu. Hapa kuna maneno mawili yenye kushindana: *kipofu* na *kilema.* Tukiangalia Ramani yetu ya kwanza ni wazi kwamba shina la Mame-Bantu, **-poku,* halikuwa katika ngeli ya KI tangu mwanzoni. Inanonekana kwamba kuingizwa kwake katika ngeli hii kumetokea katika sehemu mbili: katika lugha za Afrika Kusini—lugha hizi zinatumia ngeli ya KI kwa namna ya pekee, na katika eneo la Kiswahili. Sasa tuangalie Ramani yetu ya pili inayoonyesha ngeli za shina **-lémá* lenye maana ya 'mtu mlemavu'. Ni wazi kwamba ngeli ya KI imesambaa sana katika eneo zima la Kibantu. Lugha nyingi zinatumia *ki-lema* hivyo hivyo kilivyo, wakati lugha nyingine zikiwa na dalili za matumizi ya zamani yenye kuhusiana na ngeli hii. Tuongeze mfano mwingine. Katika lugha ya Kinyarwanda na lugha nyingine za jirani, kilema anaitwa *ikimuga.* Shina *-muga* ni mpya, lakini ngeli yake inafuata mfano wa neno la kale, *kilema.* Kwa hiyo tunapendekeza ikubalike kwamba shina hili **-lémá* lilitumiwa katika ngeli ya KI tangu zama za Mame-Bantu. Tunapendekeza pia kwamba neno *ki-lema* lilikuwa kiini cha kijopo cha maana na kuvuta majina ya walemavu wengine kama vile *kipofu, kiziwi* na wengineo. Si vigumu kufahamu ni kwa nini baadhi ya lugha zimebadilisha ngeli hii kuwa ni ngeli ya MTU/WATU.

Katika baadhi ya lugha shina **-lémá* linatokea katika nomino zenye maana 'kasoro ya mwili' au 'ulemavu'. Ramani ya tatu inaonyesha ngeli za nomino hizi katika eneo la Kibantu. Tunaona kwamba kunatumiwa ngeli mbili: ngeli ya KI na ngeli ya BU (kwa Kiswahili: U). Maneno katika ngeli ya KI kwa jumla huwa na umbo la *ki-lema;* lakini maneno katika ngeli ya BU kwa kawaida huwa na umbo linalofanana na *u-lemavu,* yaani hayatoki kwa shina *-lema* moja kwa moja lakini hutoka kwa kitenzi *ku-lema(l)a.* Kutokana na hii tunahitimisha kwamba maana nyingine ya neno **ki-lémá* katika Mame-Bantu ilikuwa 'kasoro ya mwili'.

Katika lugha ya Kiswahili, neno *kilema* lina maana hizo mbili: "1. kasoro iliyoko kwenye kiungo au viungo vya mwili; uatilifu. 2. mtu mwenye upungufu wa kiungo k.v. kiwete n.k." (TUKI 1981). Ramani yetu ya nne inaonyesha maana hizo mbili za neno *ki-lema* (katika ngeli

**Ramani 1: **-poku***




▲ ngeli 1+9


◇ ngeli 9

○ ngeli 5

△ ngeli 1


□ ngeli 7

**Ramani 2: **-lémá* (mtu)**





- ▲ ngeli 1+kitenzi
- △ ngeli 1
- ○ ngeli 5
- ▽ ngeli 3
- ▪ ngeli 1+nya+7
- ▣ ngeli 1+7
- □ ngeli 7

**Ramani 3: **-lémá* (kasoro/hali)**



**Ramani 4: **ki-lémá***




■ kasoro

◧ kasoro & mtu

□ mtu

ya KI). Sasa swali ni: je, ni maana ipi ilikuwa ya kwanza: 'kasoro ya ulemavu' au 'mtu mlemavu'? Tukikumbuka mbinu za kutunga majina ya walemavu katika ngeli ya KI tunaelewa kwamba kuna njia pana ya metonimia kutoka kasoro hadi mtu mlemavu. Kwa hiyo tunahitimisha kwamba maana ya asili ya neno *ki-lema* ilikuwa 'kasoro ya mwili'.

Sasa tunaweza kujibu swali letu "ubaguzi au heshima". Tunafikiri si ubaguzi wala si heshima kumtaja mtu kwa kutumia tabia au sifa au hata kasoro fulani. Ni mbinu ya kawaida ya kibinadamu kutumia maneno na kueneza maana zake kwa njia ya metonimia.

## 7. Uchambuzi wa mfano: *Kigego* (AYM)

*Neno "kigego" kama lilivyotumiwa zamani katika jamii ya Vaasu (Wapare):*

Hapo zamani, jamii ya Vaasu ilifuata mila na desturi ambazo ilikuwa sharti kila mwanajamii azifuate na kuzitekeleza. Moja ya jambo lililoheshimiwa sana katika mila hizo lilihusu uotaji wa meno ya kwanza ya mtoto. Kwa kawaida mtoto alitakiwa aote meno yake ya kwanza kwa kufuata utaratibu uliozoeleka, yaani meno mawili ya mbele katika taya la chini yanaota kwanza, kisha yanafuatwa na meno mawili ya mbele ya taya la juu. Baada ya meno hayo manne kuota vema, mtoto huyo hupambwa vizuri sana kama bibi harusi na hutembezwa kwa majirani na watu wote katika ukoo humshangilia sana. Wakina mama humwinua juu na kusema, *"Mwana atoroka ikamba"* wakimaanisha kwamba, mtoto amesalimika kwa kuuepuka ule mwamba wa mauti". Mtoto hupewa zawadi nyingi kwa sababu watu wanaamini kuwa mtoto amezaliwa upya.

Kama meno yataota kinyume na utaratibu huo, basi mtoto huyo hupewa jina la "kigego" na inabidi auawe (taz. Simeon 1977).

*Hatua zilizofuatwa baada ya kasoro hiyo kujulikana:*

Kigego huyu hakuuwawa wakati ule ule, ila alilelewa hadi akaweza kutambaa na hata wakati mwingine kusimama. Wazazi wa mtoto huyo pamoja na shangazi na pia bibi yake walimbeba mtoto huyo hadi porini kabisa kwenye mwamba mkubwa uliokuwa mlimani na ambao ulijulikana kwa jina la *Mkumba vana*—maana yake ni mahali pa kutupa watoto. Wazazi walihakikisha kuwa wanabeba pia mavazi ya mtoto, chungu kilichokuwa kikipikia chakula cha mtoto, sahani na bakuli alizozitumia kwa kulia chakula, kinu cha kutwangia dawa alizotumia mtoto, nguo alizokuwa akibebewa na vifaa vyote vilivyotumika katika malezi ya mtoto huyo. Walipofika katika mwamba huo walimbembeleza mtoto huyo kwa kumpa maziwa na chakula hadi alipolala usingizi. Walimlaza ukingoni kabisa mwa jabali hilo karibu sana na sehemu ya kuporomokea, yaani sehemu ambayo si salama kabisa. Pia vifaa vyote vya mtoto walivyovileta huwekwa kando yake. Baada ya hapo wazazi, shangazi na bibi hurudi nyumbani bila kutazama nyuma kama sharti moja muhimu. Sasa mtoto akiamka tu usingizini na kujisogeza kidogo, huporomoka toka juu ya mwamba ule na kufa. Ikitokea kwamba hakufa wakati ule ule, basi huuawa na kuliwa na wanyama pori kama fisi kwa sababu mwamba wenyewe upo porini kabisa.

Desturi hii ilianza kudidimia mara wamishenari walipoingia katika maeneo haya na kueneza dini ya kikristo ambayo ilikuwa kimbilio la wale wote walioona vigumu sana kutengana na watoto wao kutokana na masharti ya kimila. Mfano mmoja halisi ni kwamba kati ya Wachungaji wa kwanza wa kanisa la kilutheri huko Vuasu ya kaskazini alikuwa ni "kigego" na alitupwa kwenye mwamba ili afe. Bahati nzuri aliokolewa na kusalimishwa katika kanisa na baadaye alisomea Uchungaji.[20]

UCHAMBUZI:

*(i) Neno "kigego" lilimaanisha nini katika jamii hii?*

Tukianza na swali la kwanza tunaona kuwa katika jamii hii ya Wapare (Vaasu) jina la *kigego* lilimtaja mtoto yule mwenye kasoro fulani ya kimwili ambayo inapoonekana tu wazazi na wanajamii kwa ujumla huamini kuwa ni balaa au nuksi kwa mtoto mwenyewe na wana ukoo wote kwa pamoja. Kasoro hiyo inapogunduliwa inabidi mtoto huyo auwawe ili jamii isalimike. Ndio maana wazazi wanahakikisha kuwa mtoto huyo pamoja na vitu vinavyomhusu vinaangamizwa pamoja naye.

Hata hivyo tunafikiri kuwa, kasoro yenyewe imepewa msisitizo tu wa kiimani na jamii na wala sio kasoro ya mwili inayoonekana kama vile, kikono, kigulu au kibyongo. Tunasema hivyo kwa sababu *kigego* huyo angeachwa asiuwawe kama ilivyofanyika baadae, kusingekuwepo jinsi ya kumtambua *kigego* huyo akiwa na wenzake bila kuelezwa na mtu mwingine kuwa mtoto huyu aliotesha meno ya juu kwanza. Kwa ujumla utaona kuwa kasoro hiyo huanza tu siku ile meno ya kwanza ya juu yanapoonekana kuwa yameota kwanza kabla ya yale ya chini.

*(ii) Kwa nini neno hili limo katika ngeli ya KI?*

Kwa kujibu swali hilo tutaeleza kwa kifupi sababu zinazofanya majina ya watu yaweze kuingia katika ngeli ya KI. Kutokana na marejeo mbalimbali yanayohusu lugha za kibantu imedaiwa kuwa: (a) ngeli ya KI ni ngeli ya vitu; (b) ngeli ya namna; (c) ngeli ya udogo na pia dharau. Utaona kuwa njia za metonimia na sitiari zimetumiwa kwa watu walemavu kuingia katika ngeli hii kama vile: kutoka kitu > hadi si mtu kamili; au udogo > kuonyesha thamani ndogo; na mwisho kutoka sehemu ya mwili > kasoro yenyewe > hadi mlemavu.

*(a) Je, neno "kigego" limetumika kuonyesha udogo?*

Tunapoliangalia neno *kigego* jinsi lilivyotumika hapa ni kwamba ngeli ya KI hairejei kwenye maana ya udogo. Tunasema hivyo kwa sababu neno *gego* limefasiliwa kuwa ni 'jino la kutafunia na kusagia chakula lililoko nyuma ya kinywa'. Hivyo neno hili likitumia KI ionyeshayo udogo lingekuwa na maana ya 'gego dogo'. Kwa hali hiyo lingepoteza kabisa maana iliyokusudiwa ya kumrejea mtu, yaani mtoto aliyeotesha meno ya juu. Tunaweza

---

[20] Katika kitabu cha nyimbo, *Ngazo ya Mrungu: Kitabu cha maimbo a kukaza na kumwanjela Mrungu, Chasu he mitaso ya kikristo* (1977), Mchg. K. Nathanael Mgaya alitunga wimbo uitwao "Vana va majegho". Wimbo huo unakumbushia shida alizopata wakati alipoachwa kwenye ule mwamba wa kuulia vigego.

kusema kuwa ingawa neno *kigego–1* ('mtoto aliyeotesha meno ya juu') linafanana sana kiumbo na *kigego–2* ('gego dogo') lakini sehemu za kuliunda neno la *kigego–1* hazirejei maana zake za asili. Kwa hivyo tunaona kuwa linarejea moja kwa moja tu kumtaja mtu. Jambo la ziada ni kwamba ngeli ya kuonyesha udogo katika Chasu ni KA na wala sio KI. Kwa hivyo ina-dhihirika wazi kuwa KI imetumika kuonyesha matumizi ya namna ya upekee fulani.

*(b) Je, neno "kigego" limetumiwa katika ngeli ya KI kama metonimia au sitiari?*

Neno husemekana limetumika kimetonimia kama litataja au kuonyesha uhusiano halisi na wala sio uhusiano wa kidhanifu baina ya kitu au hali ya mtu au mtu mwenyewe (k.m. majina *kikojozi* na *kigulu* humrejea mhusika). Kuhusu sitiari ni kwamba hutaja mahusiano yasiyo halisi, ila ni yale mahusiano ya kufikiria tu; k.m. mwanamke mrembo sana hulinganishwa na upembe mdogo wa thamani nyingi wa kifaru uitwao *kipusa*.

Sasa kufuatana na maelezo yaliyotolewa hapo tunaweza kusema kuwa neno *kigego* limetumiwa katika ngeli ya KI moja kwa moja kumwita mtu bila hatua nyingine ya katikati kufuatana na kasoro iliyoonekana baada ya kuota meno ya kwanza. Hakuna muktadha ambao tunaona kuwa neno hili limetumiwa kama jina la kasoro iliyoko kwenye kiungo cha mwili. Hata katika kamusi za zamani hakuna mfano wowote uliotaja kuwa: **mtu fulani ana kigego*. Ila tunaweza kusema kuwa kigego ni namna fulani ya metonimia ya kipekee, kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| *ulimi* | > | *kilimilimi* |
| Sehemu ya mwili | > | mtu mwenye tabia ya... |

Wazo linalojitokeza hapo ni kwamba neno *kigego* linarejea kwenye metonimia, lakini metonimia hiyo inatafsiriwa kama sitiari. Hii ni kwa sababu kasoro yenyewe ni ya meno ambayo ni sehemu ya mwili. Tumesema pia kuwa metonimia hiyo ni ya kipekee kwa sababu ingekuwa ni metonimia ya kawaida jina la kasoro iliyoko mwilini lingetumika kumtaja mhusika mwenyewe.

Kama mfano tunaona kuwa kwa upande mmoja wa kimatumizi kigego linafanana na neno *kilema* ambalo limetumiwa kumtaja 'mtu mwenye upungufu au dosari fulani katika mwili', lakini pia kwa upande mwingine *kigego* linatofautiana na kilema kwa vile neno kilema linatumika pia kama jina la kasoro iliyoko mwilini.

Ili kuzidi kuona zaidi matumizi na kuenea kwa neno hili nitaonyesha jinsi neno hilo lilivyofasiliwa katika kamusi mbalimbali za Kiswahili pamoja na maandishi ya wachunguzi mbalimbali kama itakavyochambuliwa kwenye sehemu ya (iii) chini:

*(iii) Matumizi na kuenea sehemu mbalimbali kwa neno "kigego" zamani mpaka siku hizi:*

Katika jedwali hili hapa chini tunaweza kuona jinsi neno kigego lilivyotumiwa na jamii mbalimbali tofauti kama wachunguzi walivyoonyesha tokea mwisho wa karne ya kumi na tisa mpaka siku hizi. Katika jamii zote zilizotajwa hapo zimetumia neno la *kigego* kumrejea mtu moja kwa moja. Na mtu huyo aliyerejewa ni mtoto ambaye

— amezaliwa na meno yake tayari, au meno ya juu yakiwa yametokeza tayari, au
— ameotesha meno ya juu kwanza kabla ya yale ya chini.

Baadaye matumizi ya neno hili yalizidi kupanuliwa. Johnson (1939) anapanua zaidi matumizi hayo kwa kuwarejea pia watoto

— waliozaliwa katika hali isiyokuwa ya kawaida, (mf. waliotanguliza miguu kwanza; au waliozaliwa tu mara mama akafariki; na pia
— wale ambao ukuaji wao si wa kawaida.

Zaidi ya hayo utaona kuwa mtu anaweza siku hizi akatajwa kwa jina hili la *kigego* kutokana na tabia yake kama tunavyoona kwenye TUKI 1981, na Bakhressa 1992. Maana yake ya zamani ya mtoto aliyezaliwa na kasoro fulani haitumiki kwa sababu sio nuksi tena kuotesha meno ya juu kwanza, na wala sio uchimvi kuzaliwa na meno tayari na kwa hiyo mtoto huyu hauawi. Kilichobakia katika neno hili ni ile dhana iliyokuwa imejengeka katika jamii zilizotajwa ya kwamba kigego ni "balaa" au "kisirani" au kuwa "mtoto huyo atakuwa mhalifu", mkatili n.k. Kwa hivyo mtu anapotajwa kuwa ni kigego itafahamika mara moja kuwa ni mtu mwenye tabia ambazo hazikubaliki katika jamii (taz. TUKI 1981 na Bakhressa 1992). Hivyo tunaweza kusema kuwa neno hili siku hizi linatumika kama sitiari.

WASWAHILI:

Krapf 1882: mtoto aliyezaliwa na meno au meno yake ya juu yaliota kwanza; "are considered as bad omens portending distress befalling the country"; kileta. Hupelekwa msikitini na huachwa humo hadi kesho yake. Akikutwa hai ni vizuri. Asipokutwa inaaminika kuwa Mungu amembeba wakati mzuri. *"u kijego muana wewe,* thou art a villain".

Steere 1885: mtoto aliyeotesha meno ya juu kwanza; kisirani; asiye na bahati. Neno k. hutumiwa kama tusi kwa watoto wenye tabia mbaya.

Velten 1903: Mtoro bin Mwinyi Bakari:
"na iwapo mtoto ameota meno ya juu, zamani hawalei mtoto, na hatta sasa wengine hawapendi. wengine husema: 'siwezi kuitupa damu yangu, nitailea.' na wengine wanalea, lakini hawana furaha naye mtoto. na mtoto huyu huitwa kibi, maana yake 'mbaya', lakini khalafu hupewa jina kama desturi ya watoto wengine. na watu wengine hufanyiza khofu kumpa mkono mtoto huyu, sababu huchelea kufa au kuugua." (uk. 22)

Velten 1910: mtoto ambaye meno yake ya juu huota kwanza, "Unglückskind"; kibi, chimvi.

Sacleux 1939: mtoto aliyetangulia kuota meno ya juu; "enfant de malheur". *Amezaliwa kigego; Hakuzaa mwana, amezaa kigego* "...un monstre"

Johnson 1939: mtoto aoteshaye meno ya juu kwanza au aliyezaliwa katika hali isiyokuwa ya kawaida au ukuaji wake si wa kawaida. Hujulikana kama mtoto asiye na bahati; mf. *chura; chimbi; chimvi.*

Farsi 1958: "Ni uchimwi mtoto mchanga kuota meno ya juu kwanza: ni nuksi kwa wote wawili yaani kwake na kwa wazazi wake." (uk. 25)

TUKI 1981: mtoto anayezaliwa na meno yake tayari au ambaye meno yake ya juu huanza kabla ya yale ya chini; mtu asiyesikia, asiyetii la kuambiwa, asiyeonyeka.

Bakhressa 1992: mtoto mchanga anayezaliwa na meno; mtu mkaidi, asi, mhalifu; mf. Mwanawe wa kwanza alizaliwa k. lakini wa pili alizaliwa kawaida.

WANYIKA (yaani, mojawapo wa jamii Mijikenda):

Krapf 1882: mtoto aliyezaliwa na meno yake ya juu yakiwa yameshaota; kisirani, balaa. Ilisadikiwa kuwa mtoto wa aina hii huwa mhalifu au hasidi; "they are strangled by the pagan Wanika".

WAZARAMO:

Velten 1903: Mtoro bin Mwinyi Bakari: "yakitangulia meno ya juu kuota—mtoto hawamlei, watamwua ao watatafuta mtu, wanayemjua katika mji, wampe kumlea, sababu kwao si dasturi kumlea." (uk. 219)

WADOE:

Velten 1903: Mtoro bin Mwinyi Bakari: "...mtoto huyu hawamlei" (uk. 144)

WASAMBAA:

Feierman 1974: mtoto aliyeotesha meno ya juu kwanza; "a mystically dangerous being"—mtu hatari wa kimuujiza; mf. Mbegha—alinyimwa haki yake ya urithi na ndugu zake kwa sababu alikuwa kigego. (k. 43, 61, 63)

WAVIDUNDA:

Beidelman 1966: mtoto anayeotesha meno ya juu kwanza. Husadikiwa atakuwa mtundu sana na mwenye fujo; mtoto huyo hakuuwawa.

WADIGO:

Kayamba 1947: mtoto aliyeotesha meno ya juu kwanza. Mtoto huyu aliuawa kwa kutupwa mtoni na ndugu wahusika.

Swali la msingi ambalo majibu yake hatuna ni: Kwa nini jamii mbalimbali zilichukulia uotaji wa meno ya mtoto usiofuata utaratibu uliozoeleka kuwa ni balaa? Hali hii ilionekana pia huku Ulaya.[21]

*(iv) Je, matumizi ya neno "kigego" ni ubaguzi au heshima?*

Kihistoria tunaweza kuona kuwa neno *kigego* lilitumika kiubaguzi kabisa, tena wa hali ya juu. Kwa nini tunasema hivyo: Neno ubaguzi limetumiwa kumaanisha: kutenga; kubainisha.

1) Kulingana na taratibu za jamii zilizohusika mtoto aliyezaliwa *kigego* alikuwa ni mtu asiyekubalika. Ni mtu wa balaa, kisirani n.k.

21 Baldinger (1967:145) ameonyesha jinsi uotaji wa meno ya mtoto ulivyokuwa jambo la msingi katika jamii mbalimbali huku Ulaya; na pia kuhusu meno yapi yaanze. Kwa mfano: ilisemekana "Wenn das Kind den ersten Zahn im Oberkiefer bekommt, statt im Unterkiefer, so muß es bald sterben."

2) Mtu huyo alitengwa kwani wanajamii walihofia kuangamia kama wangeendelea kumtunza.

3) Jamii nyingine kama za Waasu, Wadigo n.k. vigego hao waliuawa. Kwa mfano katika jamii ya Waasu ilihakikisha kuwa inapoteza kabisa kumbukumbu zihusuzo mtoto huyo.

Na matumizi ya aina hiyo hayakuonyesha heshima kwa mhusika.

Hata kwa matumizi ya siku hizi ambapo neno hili linatumiwa kama sitiari hali ni ile ile ya kumtenga mhusika. Swala hapo ni kwamba tabia ya mhusika inayorejewa na sitiari hiyo haikubaliki na wala haivumiliwi na watu katika jamii. Tunaona kuwa bado ile imani kuhusu neno hilo haikupotea.

Kiisimu tunaweza kusema kuwa neno hili limeundwa kwa mofimu mbalimbali ikiwemo ngeli ya KI. Lakini ngeli hii hairejei kwenye hali ya udogo kwani kama tulivyoona mwanzo Chasu huonyesha hali hiyo ya udogo kwa ngeli ya KA. Inaonekana kuwa KI inaonyesha namna fulani ya kipekee. Hata hivyo mbinu hii ya kiisimu haiwezi kuelezea kwa wazi dhana hii ya ubaguzi na heshima kwa sababu wanaobagua ni *watu* na wala sio lugha. Lugha inatumika tu kama njia ya kutekelezea *matakwa* ya watu hao.

## Marejeo


Baba Malaika. 1994. *Modern Swahili–modern English.* Uchapishaji Denmark: MS-tryk.

Bakhressa, Salim K. 1992. *Kamusi ya maana na matumizi.* Nairobi: Oxford University Press.

Baldinger, Max. 1967. Aberglaube und Volksmedizin in der Zahnheilkunde. Katika *Volksmedizin,* mhariri E. Grabner, k. 116–199. Darmstadt: Wissenschaftliche Buchgesellschaft. [Tasnifu ya Ph.D., 1936; *Schweizerisches Archiv für Volkskunde.*]

Beidelman, T. O. 1966. Notes on the Vidunda of Eastern Tanzania. *Tanzania Notes and Records* 65:63–80.

Burt, F. 1910. *Swahili grammar and vocabulary.* London: S.P.C.K.

Contini-Morava, Ellen. 1995. *Noun classification in Swahili.* http://jefferson.village.virginia.edu/swahili/swahili.html

Farsi, S. 1958. *Swahili sayings from Zanzibar.* Sehemu ya 2. Nairobi: East African Publishing House.

Feierman, Steven. 1974. *The Shambaa kingdom: a history.* Madison: University of Wisconsin Press.

Givón, Talmy. 1986. Prototypes: between Plato and Wittgenstein. In *Noun classes and categorization,* mhariri C. Craig, pp. 77–102. Amsterdam: John Benjamins.

Höftmann, Hildegard, pamoja na Irmtraud Herms. 1979. *Wörterbuch Swahili–Deutsch.* Leipzig: Verlag Enzyklopädie.

Johnson, Frederick. 1939. *A standard Swahili–English dictionary.* Oxford University Press.

Kayamba, H. M. T. 1947. Notes on the Wadigo. *Tanganyika Notes and Records* 23:80–96.

Khamis, Said Ahmed Mohamed. 1984. The forgotten ki- in Kiswahili. *Lugha* 3:13–19.

Krapf, Ludwig. 1882. *A dictionary of the Suahili language*. London.

Meinhof, Carl. 1906. *Grundzüge einer vergleichenden Grammatik der Bantusprachen*. Berlin: Dietrich Reimer (Ernst Vohsen).

Miehe, Gudrun. 1977. Bemerkungen zur Lexik älterer Swahilidichtungen. *Zeitschrift der Deutschen Morgenländischen Gesellschaft*, Suppl. 3,2:1438–1460.

Mreta, Abel Y. 1996. The effect of rapid growth and predominance of Kiswahili in Tanzania. Makala yaliyosomwa kwenye 9th Swahili Colloquium, Bayreuth.

Nabhany, Ahmed Sheikh. 1978. Kandi ya Kiswahili. (Muswada.)

Newman, Paul. 1980. *The classification of Chadic within Afroasiatic*. Leiden: Universitaire Pers.

Panagl, Oswald. 1978. Agens und Instrument in der Wortbildung. Katika *Proceedings of the Twelfth International Congress of Linguists*, wahariri W. Dressler na W. Meid, k. 453–456. Innsbruck.

Polomé, Edgar C. 1967. *Swahili Language Handbook*. Washington, D.C.: Center for Applied Linguistics.

Sacleux, Charles. 1909. *Grammaire des dialectes swahilis*. Paris: Procure des PP. du Saint-Esprit.

Sacleux, Charles. 1939. *Dictionnaire swahili–français*. (Travaux et Mémoires de l'Institut d'Ethnologie, 36–37.) Paris: Musée de l'Homme.

Scheven, Albert. 1981. *Swahili Proverbs: Nia zikiwa moja, kilicho mbali huja*. Washington, D.C.: University Press of America.

Simeon, K. F. 1977. *Desturi na mila za Wapare*. Soni: Vuga Press.

Slavíková, Magdalena, na Margaret A. Bryan. 1973. The case of two Swahili dialects. *African Language Studies* 14:53-81.

Stafford, R. L. 1967. *An elementary Luo grammar*. Nairobi: Oxford University Press.

Steere, Edward. 1870. *A handbook of the Swahili language as spoken at Zanzibar*. London: Bell & Daldy. [1885: toleo la 3, limeharirishwa na kuongezwa na A. C. Madan.]

TUKI (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili). 1981. *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

TUKI (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili). 1996. *English–Swahili dictionary / Kamusi ya Kiingereza–Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Velten, Carl. 1898. *Märchen und Erzählungen der Suaheli*. Stuttgart: Spemann.

Velten, Carl. (mhariri) 1901. *Safari za Wasuaheli*. Göttingen: Vandenhoeck & Ruprecht.

Velten, Carl. (mhariri) 1903. *Desturi za Wasuaheli na khabari za desturi za sheria za Wasuaheli*. Göttingen: Vandenhoeck & Ruprecht.

Velten, Carl. 1910. *Suaheli Wörterbuch. 1. Teil: Suaheli–Deutsch*. Berlin.

Wierzbicka, Anna. 1985. *Lexicography and conceptual analysis*. Ann Arbor: Karoma Publishers.